

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 21 Mei, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Kamili Mchana)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):**

Maelezo ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F (*International Convention on Standards of Training, Certification and WatchKeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995 (STCW-1995 F)*).

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA - K.n.y. MWENYEKITI
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa

Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F (*International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995 (STCW-1995 F)*).

MHE. SUSAN L. KIWANGA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F (*International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995 (STCW-1995 F)*).

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Katibu.

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 317

Kuongeza Bajeti ya Miundombinu Masasi

MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA aliuliza:-

Mji wa Masasi unakuwa kwa kasi licha ya kutengewa kiasi cha milioni 700 kwa ajili ya miundombinu kupitia TARURA:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza bajeti hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Jimbo la Masasi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya matengenezo ya barabara katika Halmashauri ya Mji Masasi imeongezeka kutoka shilingi milioni 686.1 katika mwaka wa fedha 2018/2019 hadi shilingi milioni 860.0 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ni kuendelea kuongeza bajeti kadri makusanyo ya mapato ya Serikali yanavyoongezeka ili kukidhi matengenezo ya mtandao wa barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

Na. 318

Mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Nchini

MHE. SAED A. KUBENEA aliuliza: -

Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*) ilianzishwa kwa mtaji wa shilingi bilioni 60 tu wakati mtaji ulioidhinishwa ni shilingi bilioni 800:-

Je, hadi sasa ni kiasi gani cha mtaji kimekwishaongezwa na kukaribia mtaji ulioidhinishwa ili Benki hiyo ya Kilimo iweze kukifanya kilimo kuwa cha kisasa na endelevu?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (*TADB*) ilianzishwa kwa mtaji anzilishi wa shilingi bilioni 60.0 (*seed capital*) uliotolewa na Serikali Novemba 2014. Aidha, *TADB* imefanikiwa kujiendesha kiufanisi na kutengeneza faida kwa miaka minne mfululizo (2016, 2017, 2018 na 2019) na hivyo kukuza mtaji huo hadi kufikia shilingi bilioni 70.7 mwishoni mwa robo ya kwanza ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa *TADB* inakuwa na mtaji wa kutosha kwa ajili ya kutoa mikopo, Serikali imeipatia *TADB* kiasi cha shilingi bilioni 208 kupitia mkopo wa gharama nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) na kufanya kiasi cha mtaji uliotolewa na Serikali kufikia shilingi bilioni 268.

Kwa upande mwingine, Serikali imeipatia Benki ya *TADB* Dola za Kimarekani milioni 25.0 (sawa na shilingi bilioni 57) ili kufanya usimamizi wa Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (*Smallholder Credit Guarantee Scheme – SCGS*) chini ya mradi wa MIVARF unaosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mfuko huu unalenga kuchagiza mabanki na taasisi za fedha kuongeza ukopeshaji katika sekta ya kilimo nchini kwa kutoa dhamana kwa mikopo inayotolewa na benki na taasisi za fedha zinazoshiriki katika programu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba Benki ya *TADB* inapata fedha zaidi kwa ajili ya kukopesha, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuiwezesha benki hiyo ikiwa ni pamoja na kuitaka Menejimenti ya *TADB* kutekeleza mkakati maalum wa kutafuta fedha (*Funding Strategy*) unaolenga kutafuta fedha za gharama nafuu kutoka katika vyanzo vya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya utoaji wa mikopo na huduma nyingine muhimu katika kuchagiza maendeleo hususan katika sekta ya kilimo nchini.

Na. 319

Kigezo Kinachotumika Kupanga Bei ya Zao la Mahindi

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Serikali kupitia Shirika lake la *NFRA* imeshusha bei ya kununua mahindi toka bei ya kilo moja kwa shilingi 500 mpaka shilingi 380 kwa kilo:-

(a) Je, ni sababu zipi zimepelekea Serikali kupunguza bei ya mahindi badala ya kuongeza?

(b) Je, Serikali inaweza kuwaelekeza wakulima gharama ya kuzalisha kilo moja ya mahindi toka kuandaa shamba, kulima, kupanda, kuvuna mpaka kufikisha sokoni?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Jimbo la Kwela lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mazao hupangwa na nguvu ya soko na Serikali kupitia Wakala haijashusha bei ya mahindi. Bei zimekuwa zikibadilika kwa kuzingatia bei za soko wakati wa ununuzi wa mahindi ambapo katika msimu wa ununuzi 2019/2020 Wakala umenunua nafaka kwa bei shilingi 500 hadi shilingi 700 kwa kilo. Hata hivyo, bei za mahindi mwaka huu sokoni zimeanzia shilingi 500 mpaka shilingi 800 kwa kilo moja ya mahindi. Aidha, Wakala umekuwa ukilipa ushuru wa mazao (*produce cess*) kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa unakonunua mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kuzalisha kilo moja ya mahindi ambazo mkulima anaingia kutokana na kuandaa shamba, kulima, kupanda, kuvuna mpaka kufikisha sokoni hutofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine kutokana na utofauti wa aina ya udongo, kiasi cha pembejeo za kilimo zinazotumika, mbinu za kilimo na tija inayopatikana katika mavuno na uzalishaji. Hivyo, kutokana na tofauti ya gharama hizo, si rahisi kuelekeza gharama aina moja kwa wakulima wote. Aidha, inashauriwa wakulima kutumia Maafisa Kilimo/Maafisa Ugani wanaopatikana katika mikoa/halmashauri zao ili kubaini gharama halisi za uzalishaji kwa eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa *NFRA* imeongezewa jukumu jipya la kufanya biashara ya nafaka kwa kununua na kuuza kwa faida. Aidha, kwa kuzingatia msingi huo wa biashara, *NFRA* ina wajibu wa kununua kwa kuzingatia bei ya soko ya kununulia na kuuzia mazao yake ili

Wakala isipate hasara na kupoteza fedha za umma. Hivyo, basi kupanda na kushuka kwa bei ya mahindi inategemea nguvu ya soko kwa kuzingatia mahitaji na ugavi (*demand and supply*) na sio Serikali kupanga bei hizo.

Na. 320

Bei ya Umeme kwa Wananchi Maeneo ya Visiwani

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA aliuliza:-

Wakazi wa maeneo ya Visiwani kama vile Ukara, Irugwa na kadhalika ambao wanasambaziwa umeme na makampuni binafsi wanauziwa umeme kwa bei ya shilingi 3,500 kwa *unit* 1 ambayo ni ghali sana ukilinganisha na shilingi 1,000 kwa *unit* kwa umeme wa Gridi:-

Je, ni hatua zipi zimefikiwa na Serikali kuhakikisha wananchi hawa wanauziwa umeme kwa bei sawa na wengine?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Nishati ya mwaka, 2015 pamoja na mambo mengine inahamasisha upatikanaji wa huduma ya umeme iliyo bora na uhakika, ambapo kwa maeneo ambayo Serikali kupitia *TANESCO* haijafikisha huduma hiyo zipo Kampuni binafsi zilizoruhusiwa kutoa huduma hiyo.

Aidha, hadi kufikia Aprili, 2020 bei za kuuza umeme kwa wananchi waliounganishiwa huduma ya umeme kwenye mfumo wa Gridi ya Taifa (*TANESCO*) ni ndogo ukilinganisha na bei inayotumiwa na kampuni binafsi kuuza umeme kwa wananchi katika maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa ikiwa ni pamoja na maeneo ya Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za kulipatia ufumbuzi wa kudumu suala hilo mwezi Novemba, 2019, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

(EWURA) ilielekeza bei zote zinazotowza na TANESCO pamoja na kampuni binafsi kuwa sawa kwa maeneo yote ikiwa ni pamoja na maeneo ya Ukara na Irungwa.

Na. 321

Hitaji la REA III Namtumbo

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI aliuliza:-

Wilaya ya Namtumbo haikupata umeme kupitia Mpango wa REA I na II:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kuwa REA III inahusisha vijiji vyote vya Namtumbo?

(b) Je, ni lini umeme wa mradi wa Gridi ya Makambako – Songea utawashwa katika vijiji vilivyokusudiwa Wilayani Namtumbo?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mpango wa Serikali ni kufikisha umeme kwenye vijiji vyote vya Wilaya Namtumbo kupitia miradi ya REA Awamu ya Tatu iliyoanza kutekelezwa Julai, 2017 na kukamilika Juni, 2021. Aidha, katika Mzunguko wa Kwanza (*REA phase III Grid Extension Round I*) vijiji vipatavyo 23 vitapatiwa umeme kabla ya Juni, 2020. Vijiji hivyo ni pamoja na Utwango, Litola, Mchomoro, Luego, Namabengo, Lumecha, Nahoro, Ukiwayuyu, Kumbara, Mtakanini, Songambebe, Migelegele, Nangero, Mwinuko, Ruvuma, Nambehe, Misufini, Namahimba, Muungano, Sasawala, Liwawa, Mlalawima na Mnalawi. Vijiji vitakavyosalia vitapatiwa umeme kwenye (*REA phase III Grid Extension Round II*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji 23 inahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovolti 33 urefu wa km 56.3, njia ya umeme msongo wa kilovolti 0.4 urefu wa km 64, ufungaji wa transfoma 32 zote za kVA 50 pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 875 kwa gharama ya Dola za Marekani 657,815.10 na shilingi za bilioni 4.034.

(b) Mradi wa kuunganisha umeme wa Gridi ya Taifa wa Makambako – Songea ulikamilika Septemba, 2018 kwa kusambaza umeme katika vijiji vilivyokusudiwa Wilayani Namtumbo. Aidha, mradi ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 5 Aprili, 2019.

Na. 322

Wilaya ya Serengeti Kufaidika na Mgodzi wa ACACIA

MHE. MARWA R. CHACHA aliuliza:-

Serengeti ni moja ya Wilaya zinazoathirika na uwepo wa Mgodzi wa *ACACIA* ambao umepakana na Vijiji vya Borenga, Nyiboko na Marasomoche: -

Je, Serikali ipo tayari kuwataka *ACACIA* kutoa *Social Corporate Responsibility (CSR)* kwa vijiji hivyo pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti?

WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa ile kampuni ya *ACACIA* ilikwishanunuliwa na Kampuni ya Barrick Co. Ltd ambapo mgodzi wa North Mara kwa sasa unamilikiwa kwa ubia na Serikali kupitia Kampuni ya Twiga Co. Ltd.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 105 (1) na (2) cha Sheria ya Madini, Sura ya 123 kinamtaka mmiliki wa leseni, kuandaa mpango wenye tija wa mwaka wa wajibu wa kampuni kwa jamii uliokubalika kwa pamoja na mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika au mamlaka ya Serikali za Mtaa kwa kushauriana na Waziri anayehusika na Mamlaka za Serikali Mitaa na Waziri anayehusika na Fedha. Mgodu wa North Mara wamekuwa wakitimiza wajibu wao kwa kuandaa na kupeleka Mpango wa CSR katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kwa mujibu wa Sheria ya Madini, Sura ya 123.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2019, Mgodu uliandaa Mpango wa Utoaji Huduma wenye kiasi cha shilingi bilioni 5.75 na kupitishwa na Halmashauri ya Tarime kwa ajili ya vijiji 11 katika miundombinu ya elimu, afya, barabara na maji ambavyo ni vipaumbele vya Halmashauri ya Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa masuala ya CSR yanasimamiwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wakishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, hivyo basi, Wizara ya Madini itawasiliana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhusu pendekezo la kuwezesha Vijiji vya Borenga, Nyiboko na Marasomoche pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kunufaika na CSR inayotolewa na Kampuni ya Barrick Co.Ltd.

Na. 323

Kuwa na Njia Nyingine Mbadala za Kutambua Magonjwa

MHE. MGENI JADI KADIKA aliuliza:-

Kuna magonjwa mengi sana duniani ambayo njia zake za kuyatambua ni tofauti mbali na kutumia tochi ambazo hutumika katika *airports* na bandari:-

Je, ni hatua gani nyingine ambazo Serikali inachukua ili kuwalinda raia wake?

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeimarisha mifumo yake yote ya ufuatiliaji wa wagonjwa na matukio ya kiafya, kuanzia ngazi ya jamii, vituo vya afya na maeneo mengine zaidi ya kutumia tochi katika viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu. Mfumo huo wa ufuatiliaji hutumia simu (*mobile application*) katika kutolea taarifa ya magonjwa na matukio ya kiafya pindi yanapatokea na upo katika vituo vyote vya kutolea huduma nchini. Gharama za uendeshaji wa mfumo huu, zinatolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kumwezesha mtumishi kutumia kwa kutuma taarifa upesi/haraka kwa kutumia simu pasipo kutoa malipo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara, imeimarisha mfumo wa kufuatilia magonjwa, tetesi (*rumours*) na matukio ya afya katika ngazi ya jamii. Hii ni kwa sababu si matukio yote hufika katika vituo vya kutolea huduma. Mfumo huu ni shirikishi kwa jamii ambapo husaidia jamii kutoa taarifa kwa kupitia *toll free* namba ya Wizara au kwa watoa huduma ngazi ya jamii na kituo chochote cha afya kilicho karibu kuhusu matukio yoyote ya kiafya, tetesi au minong'ono ya kuhusu ugonjwa katika jamii yake yanayojitokeza. Aidha, wataalamu wa afya hufuatilia matukio haya ya kiafya kupitia kwenye vyombo vya habari, magazeti, mitandao ya kijamii na kadhalika ili kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya njia ambazo hutumika kutambua wagonjwa hawa ni pamoja na kuchunguza kwa kuangalia hali yake ya nje ya kiafya (*physical observation*); kumwuliza maswali kuhusu afya yake ili kutambua iwapo alikuwa katika hatari ya kupata maambukizi; kupima joto kwa kutumia vipima joto; kuchukua sampuli ili kuthibitisha iwapo ana ugonjwa na kumpima kwa kutumia *Computerized Tomography (CT) scan*. Njia hizi ndio

zinazotumika duniani kote katika kufuatilia na kutambua wagonjwa wa magonjwa mbalimbali ya milipuko.

Na. 324

Maboresho ya Vifurushi vya Bima ya Afya

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU aliuliza:-

Ili kuboresha afya ya Watanzania, Serikali iliahidi kuboresha Bima ya Afya kwa kuongeza vifurushi mbalimbali vya Bima ya Afya:-

Je, ni maboresho gani yamefanyika mpaka sasa?

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za matibabu nchini, Mfuko umeendelea kuboresha mafao yatolewayo kwa wanufaika wake pamoja na kuongeza usajili wa vituo vya huduma ikiwa ni utekelezaji wa mikakati yake ya kushawishi makundi mbalimbali ya wananchi kujiunga na kunufaika na utaratibu wa bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kama sehemu ya kuongeza ushindani wa kibiashara katika soko la bima ya afya nchini, Mfuko umeanzisha utaratibu wa kutoa huduma za ziada (*supplementary package*) kwa taasisi za umma au makampuni binafsi yanayohitaji huduma hizo. Baadhi ya huduma za ziada zinazotolewa na Mfuko ni pamoja na Huduma ya Uokozi kwa njia ya Anga, Huduma ya Gari la Wagonjwa, Huduma ya Kupima Afya, Huduma ya Matibabu nje ya nchi na huduma nyinginezo zitakazohitajika na taasisi husika kulingana na uhitaji na uwezo wa kuzilipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kujumuisha makundi mbalimbali ya wananchi katika mfumo wa bima ya afya nchini, Mfuko umeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza wigo wa wanachama katika sekta rasmi ya umma na binafsi na ile isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudi hizo, mbali ya watumishi wa umma ambao hujiunga kwa mujibu wa sheria, mikakati hii imewezesha Mfuko kujumuisha makundi mbalimbali ya wananchi ikiwemo ya wanafunzi wa vyuo na shule kupitia utaratibu wa bima ya afya kwa wanafunzi, watoto chini ya miaka 18 kupitia utaratibu wa Toto Afya Kadi, wakulima katika vyama vya msingi kupitia utaratibu wa Ushirika Afya, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, wajasiriamali wadogo ikiwemo Wamachinga, Bodaboda, Madereva, Baba na Mama Lishe, Wafanyakazi wa Makampuni Binafsi pamoja na Watu binafsi kupitia utaratibu wa vifurushi vya bima ya afya vijulikanavyo kwa majina ya Najali Afya, Wekeza Afya na Timiza Afya.

Na. 325

Kuvisaidia Viwanda Vidogo Vidogo Kukuza Ajira Mpanda

MHE. RHODA E. KUNCHELA aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvisaidia viwanda vidogo vidogo kuzalisha ajira nyingi na kukuza uchumi kwa wananchi katika Manispaa ya Mpanda?

(b) Je, Serikali ina mpango na kiwanda cha alizeti cha MPADECO ambacho hakina uwezo wa kuongeza ajira?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Manispaa ya Mpanda hadi kufikia Aprili, 2020 kulikuwa na jumla ya viwanda vidogo 476 na Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuvisaidia viwanda hivyo ili viweze kukuza uchumi na kuzalisha ajira kwa wananchi. Mikakati iliyotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kutenga eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 120,670.2 sawa na ekari 30 katika kata ya Misunkumilo. Eneo hilo tayari lina miundombinu ya maji, umeme, choo na kibanda cha mlinzi. Hadi kufikia Machi, 2020 jumla ya viwanda vidogo vidogo 42 vimeanzishwa na kutoa ajira 200;

(ii) Kutoa elimu ya biashara na mafunzo ya usindikaji wa vyakula ili kuongeza thamani mazao ya kilimo;

(iii) Kusaidia upatikanaji wa teknolojia rafiki kwa ajili ya uongezaji thamani mazao kama karanga, alizeti, mpunga, ufuta na asali;

(iv) Kutambua na kurahisisha viwanda vidogo ili vizalishe katika kiwango bora pia kuvipatia leseni za biashara na maelekezo mahsusi na taratibu za uendeshaji wa viwanda;

(v) Kutoa mikopo kwa viwanda vidogo vidogo na kutenga 10% ya mapato ya ndani kuwezesha vikundi vya ajira, wanawake na walemavu; na

(vi) Ili kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa zinayafikia masoko kwa ufanisi miundombinu ya barabara imeimairishwa na barabara zifuatazo zinajengwa/zimejengwa kwa kiwango cha lami:

(a) Kuanzia Sumbawanga hadi Mpanda imejengwa kwa kiwango cha lami;

(b) Kuanzia Tabora hadi Mpanda inajengwa kwa kiwango cha lami; na

(c) Kuanzia Mpanda hadi Kigoma inajengwa kwa kiwango cha lami.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda (Tanganyika) imetenga kiasi cha shilingi milioni 50 katika mwaka 2020/2021 kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na kufanya ukarabati wa kiwanda cha MPADECO. Baada ya ukarabati na uboreshaji wa kiwanda hicho, ajira kwa wananchi zitapatikana na wakulima watakuwa na uhakika wa soko la alizeti.

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI

HOJA ZA SERIKALI

Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F (*International Convention on Standards of Training, Certification and WatchKeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimuite Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kwa niaba yake Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI - K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Bunge la lako tukufu naomba kuwasilisha maelezo kuhusu mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F (*International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995*).

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha

kukutana tena katika Bunge lako Tukufu tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kusimamia kwa ufanisi majadiliano yote yaliyofanyika katika kipindi chote cha Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Shirika la Bahari Duniani (*International Maritime Organisation-IMO*). Lengo la kuanzishwa kwa Shirika hilo ni pamoja na kuweka miongozo, viwango vya ulinzi na usalama kwa watu, vyombo vya majini, mali pamoja na taratibu za usimamizi wa viwango hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 unalenga kusimamia viwango vya mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi vyenye urefu wa kuanzia mita 24 na kuendelea vinavyotumika katika shughuli za uvuvi katika maji ya ndani na nje ya mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 1994, kazi ya uvuvi ilionekana kuwa ni kati ya kazi hatari duniani ambazo ni hatari na kusababisha vifo vya wavuvi 24,000. Idadi hii ni zaidi ya mara 10 ya vifo vinavyotokea katika meli za biashara (merchant ships). Kwa mujibu wa Taarifa za Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), hadi kufikia mwaka 1977, ilionekana pia kuwa wafanyakazi wa meli za uvuvi hufanya kazi kwa saa nyingi zaidi bila kuzingatia masharti ya ajira na bila kuwa na vitendea kazi bora. Hata hivyo, Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (*FAO*) limekuwa likitoa taarifa za meli kufanya kazi za uvuvi haramu usiotumia vifaa na kwa kutozingatia maelekezo ambapo ni kinyume na taratibu za kisheria za Kimataifa. Kutokana na kukosekana kwa uhibitaji wa kutosha, Umoja wa Mataifa kupitia Wakala zake iliandaa Mikataba na Itifaki mbalimbali kuhusu usalama wa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 unaweka viwango vya kimataifa vya mafunzo na utoaji wa vyeti kwa wafanyakazi katika vyombo vya uvuvi. Viwango vilivyopangwa vinawahusu Nahodha, Maofisa, Wahandisi wa Meli, Maofisa wa Mawasiliano na Wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa ya kupitishwa kwa Azimio hili ni pamoja na kuwezesha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi kutoa mafunzo na vyeti vinavyotambulika kimataifa katika uvuvi wa vyombo vya bahari kuu. Vyuho vilivyoko hapa nchini kwa sasa ni pamoja na Bagamoyo (Pwani), Nyegezi (Mwanza), Kibirizi (Kigoma), Rorya (Mara) na Mikindani (Mtwara).

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya madhara yanayoweza kutokea iwapo Mkataba huu hautaridhiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Watanzania kutoajirika katika nafasi za kimataifa katika eneo la uvuvi wa bahari kuu, kinyume na wale wanaofanya kazi katika meli za biashara;

(b) Kukosa nguvu za ukaguzi na uangalizi wenye weledi kwa meli za Kimataifa zinazofanya kazi katika bahari kuu kwa ajili ya kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari;

(c) Kukosekana kwa usimamizi wa ulinzi, usalama na uchafuzi wa mazingira ya bahari;

(d) Tanzania kutoonekana kuwa eneo salama la kuvua samaki kwa kutofikia viwango vya kimataifa; na

(e) Nchi kukosa mapato kutokana na kukosekana kwa ajira za Watanzania katika soko la kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu muhimu vilivyoainishwa katika Mkataba huu ni pamoja na vifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 1, wajibu wa nchi wanachama. Ibara hii inaeleza kuwa nchi wanachama wa Mkataba huu zinawajibika kutekeleza ipasavyo ibara zote na viambatisho vya Mkataba huu. Aidha, zinatakiwa kutekeleza sheria, kanuni na taratibu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 2, tafsiri ya maneno. Ibara hii inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 3, matumizi ya Mkataba. Ibara hii inabainisha kuwa Mkataba huu utawahusu wafanyakazi walioko katika vyombo vya uvuvi baharini vinavyovua ndani na nje ya mipaka ya maji ya nchi vilivyosajiliwa kisheria na vinapeperusha bendera ya nchi mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4, utoaji wa taarifa. Ibara hii inaitaka kila nchi mwanachama kutoa taarifa za utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 5, Mikataba mingine na tafsiri zake. Ibara hii inaitaka Mikataba, Itifaki na taratibu zilizoidhinishwa kuhusiana na Mkataba huu kuendelea kutambulika. Pale ambapo itabainika kuwa Mkataba huu unagongana na Mikataba au Itifaki za nchi mwanachama, nchi mwanachama itabidi kupitia upya Mikataba na Itifaki hizo ili kuondoa migongano hiyo. Masuala yote ambayo hayajaelezwa katika Mkataba huu, yatekelezwa kwa kuzingatia sheria za nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6, utoaji wa vyeti. Ibara hii inawataka wafanyakazi katika vyombo vya uvuvi kupewa vyeti vya mafunzo kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 7, utaratibu wa uchunguzi. Ibara hii inaitaka nchi wanachama pamoja na mambo mengine, kuweka utaratibu wa kuchunguza vitendo

vilivyotolewa taarifa vinavyohatarisha au kutishia usalama wa watu, rasilimali za bahari na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 8, taratibu za udhibiti. Ibara hii inazitaka vyombo vya uvuvi vinapokuwa katika bandari ya kuu kuzingatia taratibu zote za udhibiti kama Mkataba huu unavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 9, kuimarisha ushirikiano wa nchi wanachama. Ibara hii inabainisha kuwa nchi wanachama zitaimarisha ushirikiano na misaada kwa nchi wanachama kulingana na Mkataba huu unavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10, marekebisho ya Mkataba. Ibara hii inaruhusu Mkataba huu kufanyiwa marekebisho kwa nchi mwanachama kuwasilisha mapendekezo kwa Katibu Mkuu wa *International Maritime Organisation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12, kuanza kutumika kwa Mkataba. Ibara hii inahusu kuanza kutumika kwa Mkataba huu miezi 12 baada ya Mkataba kuridhiwa na nchi wanachama zisizopungua 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13, kujitoka katika uanachama wa Mkataba. Ibara hii inatoa fursa ya nchi mwanachama kujitoka katika Mkataba baada ya miaka mitano tangu tarehe ya kujiunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14, uwasilishaji wa Hati ya Kuridhia Mkataba. Ibara hii inaeleza kuwa Hati ya Kuridhia Mkataba itawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa *IMO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuwasilisha Azimio hili kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Nchi Wanachama wa Shirika la Bahari Duniani (*International Maritime Organisation - IMO*) ziliandaa Mikataba na Itifaki mbalimbali ikiwemo Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F uliosainiwa tarehe 7 Julai, 1995 mjini London, Uingereza na kuanza kutumika tarehe 29 Septemba, 2012.

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu mwaka 1974 ni mwanachama wa Shirika la Bahari Duniani (*International Maritime Organization* lilloanzishwa tarehe 17 Machi, 1948 na ambalo ni miongoni mwa mashirika ya Umoja wa Mataifa.

NA KWA KUWA lengo kuu la kuanzishwa kwa shirika hilo ni kuweka viwango vya ulinzi na usalama wa watu na vyombo vya majini pamoja na uhifadhi wa mazingira ya bahari.

NA KWA KUWA katika kusimamia majukumu yake *IMO* imekuwa ikiandaa Mikataba na Itifaki mbalimbali ikiwemo Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F (*International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995* unaopendekezwa kuridhiwa;

NA KWA KUWA Mkataba huu unafuatia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Viwango vya Mafunzo na Utoaji Vyeti kwa Mabaharia wa Mwaka 1978 na marakebisho yake ulioridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1984 (*International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Seafarers, 1978 as amended*) ambao ni maalum kwa ajili ya kusimamia na kudhibiti viwango vya mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya baharini;

NA KWA KUWA Mkataba wa mwaka 1995 una lengo la kuweka, kusimamia na kudhibiti viwango vya kimataifa vya mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi katika vyombo vya

uvuvi vyenye urefu wa kuanzia mita 24 na kuendelea vinavyotumika katika shughuli za uvuvi;

NA KWA KUWA kuridhiwa kwa Mkataba huu kutawezesha vyyo vya mafunzo vyenye ithibati ya kutoa elimu ya mafunzo ya uvuvi yenye viwango vya kimataifa na kutayarisha wataalam wenye weledi watakaotumia kazi hizo;

NA KWA KUWA kuridhiwa kwa Mkataba huu kutakuwa na manufaa yafuatayo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

(i) Kutoa fursa za ajira za ndani na za kimataifa kwa wataalam wa vyombo vya uvuvi;

(ii) Kuwepo kwa wakaguzi na waangalizi (*inspectors and observers*) wenye weledi ambao kuwepo kwao kutahakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari;

(iii) Kutaimarisha vyyo vya ndani vya mafunzo ya uvuvi na kutambulika kimataifa;

(iv) Kuwepo kwa viwango bora vya ufundishaji kwa wanafunzi;

(v) Kuimarisha usalama wa wafanyakazi katika vyombo vya uvuvi na hivyo kupunguza ajali;

(vi) Kuimarika kwa ulinzi, usalama na uhifadhi wa mazingira ya bahari; na

(vii) Kuimarishwa kwa upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali katika sekta ya uvuvi.

HIVYO BASI kwa kuzingatia manufaa yatakayopatikana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na Mkataba huu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Tisa na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia

Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F (*The International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessels Personnel, 1995*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Hawa Mchafu.

MHE. HAWA M. CHAKOMA - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F (*International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995 (STCW-F-95)*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Nyongeza ya Nane, kifungu cha 7(1)(b) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inazipa Kamati za Bunge za kisekta ikiwemo Kamati ya Miundombinu, jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba iliyo chini ya Wizara inazozisimamia na inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge. Jukumu hili pia ni la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995. Chimbuko la Mkataba huu ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mwanachama wa Shirika la Bahari Duniani (*International Maritime Organization*) lililoanzishwa tarehe 17 Machi, 1948. Shirika hili linajielekeza katika shughuli za bahari, usalama baharini, usafirishaji mizigo Kimataifa pamoja na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira baharini. Lengo la Shirika hili ni kuweka viwango vya ulinzi na usalama wa watu na vyombo vya majini pamoja na uhifadhi wa mazingira ya bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba unalenga mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi vyenye urefu wa kuanzia mita 24 na kuendelea vinavyotumika katika shughuli za uvuvi kwenye maji ya ndani na nje ya mipaka ya nchi. Kwa jumla, Mkataba huu unawahusu wafanyakazi wa meli za uvuvi, wamiliki wa meli hizo, vyuo au taasisi za mafunzo pamoja na nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na chimbuko la Mkataba huu kuwa ni Tanzania kuwa mwanachama wa Shirika la Bahari Duniani, itakumbukwa kuwa tarehe 17 Novemba, 2017, Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, aliunda Kamati Maalum ya Bunge ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Uvuvi wa Bahari Kuu nchini. Kamati hiyo ilisoma taarifa yake ambayo pia ilikabidhiwa Serikalini tarehe 15 Mei, 2018 na kubainisha kuwa pamoja na mambo mengine, Tanzania ina changamoto za utaalumu na weledi wa shughuli za uvuvi wa bahari kuu na hivyo kuathiri majukumu ya msingi ya kila siku ya uvuvi wa bahari kuu kama vile waangalizi wa meli jambo ambalo linachangia upotevu wa mapato, kukosekana kwa takwimu sahihi za uvuvi wa bahari kuu pamoja na uwepo wa ukiukwaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa matokeo hayo, Kamati ilipendekeza maboresho makubwa kwenye mfumo na uendeshaji wa shughuli za uvuvi wa Bahari Kuu nchini ikiwemo kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa katika masuala ya uvuvi

pamoja na maboresho ya sheria na kanuni za uvuvi wa bahari kuu. Hivyo, hatua za Serikali kuleta Mkataba huu Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa ni mojawapo ya hatua za kufanyia maboresho mfumo wa shughuli za Uvuvi wa Bahari Kuu kama ilivyoshauriwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuridhia mkataba huu faida mbalimbali zitapatikana nazo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kutoa fursa za ajira za ndani na za Kimataifa kwa wataalamu wa vyombo vya ndani vya uvuvi;

(b) Kuwapo kwa Wakaguzi na Waangalizi wenye weledi ambapo kuwepo kwao kutahakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari;

(c) Kuimarisha vyo vya ndani vya mafunzo ya uvuvi na kutambulika Kimataifa;

(d) Kuwepo kwa viwango bora vya ufundishaji wanafunzi katika Vyo vya Uvuvi nchini;

(e) Kuimarisha usalama wa wafanyakazi katika vyombo vya uvuvi na hivyo kupunguza ajali;

(f) Kuimarika kwa ulinzi, usalama na uhifadhi wa mazingira ya bahari; na

(g) Kuimarika kwa upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali katika Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishughulikia hoja hii katika hatua tatu kama ifuatavyo:-

(a) Kupokea maelezo ya sekretarieti kuhusu dhana na uchambuzi wa kisheria wa Mkataba;

(b) Kupokea maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la kuridhia Mkataba. Maelezo hayo yalifanua nia ya Serikali katika kuingia kwenye mkataba huu imesukumwa na hitaji

la kuweka mazingira wezeshi ambayo yataleta utatuzi wa changamoto zilizopo katika sekta nzima ya uvuvi wa bahari kuu kama vile vifo, wafanyakazi wa meli za uvuvi kufanya kazi pasipo staha ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwa saa nyingi zaidi pasipo kuzingatia masharti ya ajira, kufanya kazi pasipo vitendea kazi, uvuvi haramu kwa kutokutumia vifaa vya uvuvi, kutotoa taarifa za uvuvi, uvuvi usiodhibitiwa na mazao mengi ya uvuvi kuuzwa kwa njia haramu; na

(c) Kupokea maoni ya wadau, pamoja na Wajumbe kuchambua na kutoa maoni kuhusu Mkataba huu na hatimaye kuishauri Serikali lengo la kuboresha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitoe maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Mkataba huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni:-

(a) Ibara za Mkataba ambazo jumla yake zipo kumi na tano zinazoainisha wajibu wa kisheria ambao unatakiwa kutekelezwa na nchi wanachama;

(b) Kiambatisho ambacho kinaweka ufafanuzi wa masuala ya kitaalamu yanayohusu utekelezaji wa ibara za mkataba; na

(c) Kanuni ambazo zinafafanua masuala ya kitaalamu ambayo ni lazima yaeklezwe na nchi mwanachama na masuala ambayo utekelezaji wake ni wa hiyari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imepitia na kuchambua mkataba huu ibara kwa ibara na kutoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

(a) Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kuleta Azimio hili la kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo na Utoaji Vyeti kwa Wafanyakazi wa Vyombo vya Uvuvi wa Mwaka 1995. Ni muhimu Serikali kuzingatia mikataba ambayo ni mizuri na yenye faida kwa nchi yetu na kuiwasilisha Bungeni

ili kuridhia mapema na kuanza kunufaika badala ya kusubiri athari zitokee.

(b) Kwa kuwa Ibara ya 15 ya mkataba inahusu lugha ya mkataba kuwa ni lugha sita ambapo nakala iliyo katika lugha hizo itachukuliwa kuwa ni halisi. Lugha hizo ni Kiarabu, Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kirusi na Kihispaniola. Kamati inaona umuhimu wa Serikali kupeleka mapendekezo ya kuingiza lugha ya Kiswahili kwa kuwa ni lugha ya Kimataifa ambapo nchi zilizopo kusini mwa Afrika ambazo zina utajiri mkubwa wa bahari zimeamua kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya Kimataifa.

(c) Kwa kuwa mkataba huu unalenga kuimarisha na kuweka viwango vya ulinzi na usalama wa watu na vyombo vya majini, ni muhimu sana Serikali iharakishe kuandaa Sera ya bahari kwani Sera hii ni muhimu sana hasa kama nchi inataka kuwekeza na kunufaika na uchumi unaotokana na bahari.

(d) Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (*TASAC*) liimarishwe na kuboreshwa kwa kuhakikisha linakuwa na vyombo ama vitendea kazi bora na vyenye kukidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa kwenye kufanya kaguzi.

(e) Katika kuhakikisha kuwa Mkataba huu unatekelezwa ipasavyo, ni muhimu Serikali kuangalia sheria mbalimbali zilizopo na kuona kama zinaweza kukidhi mawanda ya mkataba huu na ikiwa baadhi zitakuwa zinakinzana, ziweze kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika,

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya ya Shirika la Bahari Duniani (*IMO*) tangu mwaka 1974;

NA KWA KUWA, kati ya nchi 174 wanachama wa Shirika la Bahari Dunia ni nchi 33 zilizoridhia Mkataba huu ambapo kati ya nchi hizo, nchi za Afrika ni tisa ambazo ni

Uganda, Congo, Gambia, Sierra Leone, Afrika Kusini, Namibia, Morocco, Tunisia na Mauritius;

NA KWA KUWA, Tanzania kuridhia mkataba huu kutapatikana faida mbalimbali zikiwemo ajira za ndani na za Kimataifa, kuwa na wakaguzi na waangalizi wenye weledi, kuimarika kwa ulinzi na usalama wa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi na kuimarika kwa upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali katika Sekta ya Uvuvi;

HIVYO BASI, kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Viwango vya Mafunzo na Utoaji wa Vyeti kwa Wafanyakazi wa Vyombo vya Uvuvi wa Mwaka 1995 (*International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995*) ili kulingana na nchi wanachama wenzetu kwa kuzingatia manufaa yatakayotokana na mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa wasaa wa kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Eng. Isack Alloyce Kamwelwe, Manaibu Waziri Mheshimiwa Eng. Atashasta Justus Nditiye pamoja na Mheshimiwa Elias John Kwandikwa. Vilevile, nawashukuru Katibu Mkuu wa Sekta ya Uchukuzi Eng. Dkt. Leonard Chamurio na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Rashid A. Tamatamah na Watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika vikao na kutoa maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati kuchambua Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa ushirikiano na mchango wa mawazo wakati wote wa kutekeleza kazi hii hadi kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa ruhusa yako naomba majina yao yote yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.
(*Makofi*)

**AZIMIO LA BUNGE KUHUSU MAPENDEKEZO YA KURIDHIA
MKATABA WA KIMATAIFA WA VIWANGO VYA MAFUNZO NA
UTOAJI VYETI KWA WAFANYAKAZI WA VYOMBO VYA UVUVI
WA MWAKA 1995 (INTERNATIONAL CONVENTION ON
STANDARDS OF TRAINING, CERTIFICATION AND
WATCHKEEPING FOR FISHING VESSEL PERSONNEL, 1995) -
KAMA ILIVYOWSILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, na kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkatoba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo na Utoaji Vyeti kwa Wafanyakazi wa Vyombo vya Uvuvi wa Mwaka 1995 [*International Convetion on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessel Personel, 1995 (STCW-F-95)*].

Mheshimiwa Spika, katika nyongeza ya nane, kifungu cha 7(1) (b) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inazipa Kamati za Bunge za kissekta ikiwemo Kamati ya Miundombinu, jukumu la kushughulikia miswada ya sheria na Mikataba iliyo chini ya Wizara inazozisimamia na inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge. Jukumu hili pia ni la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

1.1 Chimbuko la Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo na Utoaji Vyeti kwa Wafanyakazi wa Vyombo vya Uvuvi wa Mwaka 1995

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Mkataba huu ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mwanachama wa Shirika la Bahari Duniani (*International Maritime Organization*) lililoanzishwa tarehe 17, Machi 1948. Shirika la hili linajielekeza katika shughuli za bahari, usalama baharini, usafirishaji mizigo Kimataifa pamoja na udhibiti wa uchafuzi wa Mazingira baharini. Lengo la Shirika hili ni kuweka viwango vya ulinzi na usalama wa watu na vyombo vya majini pamoja na uhifadhi wa mazingira ya bahari.

Mheshimiwa Spika, mkataba unalenga mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi vyenye urefu wa kuanzia mita 24 na kuendelea vinavyotumika katika shughuli za uvuvi kwenye maji ya ndani na nje ya mipaka ya nchi. Kwa jumla, Mkataba huu unawahusu wafanyakazi wa meli za uvuvi, wamiliki wa meli hizo, vyo au taasisi za mafunzo pamoja na nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na chimbuko la Mkataba huu kuwa ni Tanzania kuwa mwanachama wa Shirika la Bahari Duniani, itakumbukwa kuwa tarehe 17 Novemba, 2017 Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mb aliunda Kamati Maalum ya Bunge ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Uvuvi wa Bahari Kuu nchini. Kamati hiyo ilisoma taarifa yake ambayo pia ilikabidhiwa Serikalini tarehe 15 Mei, 2018 na kubainisha kuwa, pamoja na mambo mengine, Tanzania ina changamoto za utaalumu na weledi wa shughuli za uvuvi wa bahari kuu na hivyo kuathiri majukumu ya msingi ya kila siku ya uvuvi wa bahari kuu kama vile waangalizi wa meli jambo ambalo linachangia upotevu wa mapato, kukosekana kwa takwimu sahihi za uvuvi wa bahari kuu pamoja na uwepo wa ukiukwaji wa sheria.

Kwa matokeo hayo, Kamati ilipendekeza maboresho makubwa kwenye mfumo na uendeshaji wa shughuli za uvuvi wa bahari kuu nchini ikiwemo kuimarisha ushirikiano wa

kimataifa katika masuala ya uvuvi pamoja na maboresho ya sheria na kanuni za uvuvi wa bahari kuu. Hivyo, hatua za Serikali kuleta Mkataba huu Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa ni mojawapo ya hatua za kufanyia maboresho ya mfumo wa shughuli za uvuvi wa bahari kuu kama ilivyoshauriwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuridhia Mkataba huu, faida mbalimbali zitapatika naambazo ni: -

- a) Kutoa fursa za ajira za ndani na za kimataifa kwa wataalamu wa vyombo vya ndani vya uvuvi;
- b) Kuwapo kwa wakaguzi na waangalizi wenye weledi ambapo kuwepo kwao kutahakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari;
- c) Kuimarisha vyuo vya ndani vya mafunzo ya uvuvi na kutambulika kimataifa;
- d) Kuwepo kwa viwango bora vya ufundishaji wa wanafunzi katika vyuo vya uvuvi nchini;
- e) Kuimarisha usalama wa wafanyakazi katika vyombo vya uvuvi na hivyo kupunguza ajali;
- f) Kuimarika kwa ulinzi, usalama na uhifadhi wa mazingira ya bahari; na
- g) Kuimarika kwa upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali katika sekta ya uvuvi.

1.2 Namna Kamati ilivyoshughulikia Azimio

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishughulikia hoja hii katika hatua tatu zifuatazo: -

- a) Kupokea maelezo ya Sekretarieti kuhusu dhana na uchambuzi wa kisheria wa Mkataba;

b) Kupokea maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la kuridhia Mkataba. Maelezo hayo yalifafanua nia ya Serikali kutaka kuingia kwenye mkataba huu imesukumwa na hitaji la kuweka mazingira wezeshi ambayo yataleta utatuzi wa changamoto zilizo katika sekta nzima ya uvuvi wa bahari kuu kama vile vifo, wafanyakazi wa meli za uvuvi kufanya kazi pasipo staha ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwa saa nyingi zaidi pasipo kuzingatia masharti ya ajira, kufanya kazi pasipo vitendea kazi, uvuvi haramu kwa kutokutumia vifaa vya uvuvi, kutotoa taarifa za uvuvi, uvuvi usiodhibitiwa na mazao mengi ya uvuvi kuuzwa kwa njia haramu;na

c) Kupokea maoni ya wadau, pamoja na wajumbe kuchambua na kutoa maoni kuhusu Mkataba huu na hatimaye kuishauri Serikali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wake.

2.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni:

a) Ibara za Mkataba ambazo jumla yake zipo kumi na tano zinazoainisha wajibu wa kisheria ambao unatakiwa kutekelezwa na nchi wanachama;

b) Kiambatisho ambacho kinaweka ufafanuzi wa masuala ya kitaalamu yanayohusu utekelezaji wa ibara za mkataba; na

c) Kanuni ambazo zinafafanua masuala ya kitaalamu ambayo ni lazima yatekelezwe na nchi wanachama na masuala ambayo utekelezaji wake ni wa hiyari.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia na kuchambua Mkataba huu ibara kwa ibara, na kutoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo; -

a) Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kuleta Azimio hili la kuridhia

Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo na Utoaji Vyeti kwa Wafanyakazi wa Vyombo vya Uvuvi wa Mwaka 1995. Ni muhimu kwa Serikali kuzingatia mikataba ambayo ni mizuri na yenye faida kwa nchi yetu na kuiwasilisha Bungeni ili kuridhiwa mapema na kuanza kunufaika badala ya kusubiri athari zitokee.

b) Kwa kuwa Ibara ya 15 ya mkataba inahusu lugha ya mkataba kuwa ni lugha sita ambapo nakala iliyo katika lugha hizo itachukuliwa kuwa ni halisi. Lugha hizo ni Kiarabu, Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kirusi na Kihispaniola. Kamati inaona umuhimu wa Serikali kupeleka mapendekezo ya kuingiza lugha ya Kiswahili kwa kuwa ni lugha ya Kimataifa, ambapo nchi zilizopo kusini mwa Afrika ambazo zina utajiri mkubwa wa bahari zimeamua kuifanya lugha ya Kimataifa.

c) Kwa kuwa Mkataba huu unalenga kuimarisha na kuweka viwango vya ulinzi na usalama wa watu na vyombo vya majini. Ni muhimu sana Serikali iharakishe kuandaa Sera ya bahari kwani Sera hii ni muhimu sana hasa kama nchi inataka kuwekeza na kunufaika na uchumi unaotokana na bahari.

d) Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania-TASAC liimarishwe na kuboreshwa kwa kuhakikisha linakuwa na vyombo/vitendea kazi bora na vyenye kukidhi viwango vya Taifa na Kimataifa kwenye kufanya kaguzi.

e) Katika kuhakikisha kuwa Mkataba huu unatekelezwa ipasavyo, ni muhimu Serikali kuangalia sheria mbalimbali zilizopo na kuona kama zinaweza kukidhi mawanda ya Mkataba huu na ikiwa baadhi zitakuwa zinakinzana ziweze kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya ya Shirika la Bahari Duniani-IMO tangu mwaka 1974. Na kwa kuwa kati ya nchi 174 wanachama wa Shirika la Bahari Dunia ni nchi 33 zilizoridhia Mkataba huu ambapo kati ya nchi hizo, nchi za Afrika ni tisa ambazo ni Uganda, Congo, Gambia, Sierra Leone, Afrika Kusini, Namibia, Morocco, Tunisia na Mauritius.

Na kwa kuwa kwa Tanzania kuridhia mkataba huu kutapatikana faida mbalimbali zikiwemo ajira za ndani na za kimataifa, kuwa na wakaguzi na waangalizi wenye weledi, kuimarika kwa ulinzi na usalama wa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi na kuimarika kwa upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali katika sekta ya uvuvi.

Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Viwango vya Mafunzo na Utoaji wa Vyeti kwa Wafanyakazi wa Vyombo vya Uvuvi wa Mwaka 1995 (*International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995*) ili kuungana na nchi wanachama wenzetu kwa kuzingatia manufaa yatokanayo Mkataba huu.

3.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa wasaa wa kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha naomba nimshukuru Naibu Spika pamoja na wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Eng. Isack Alloyce Kamwelwe, Mb, Manaibu Waziri Mheshimiwa Eng. Atashasta Justus Nditiye, Mb pamoja na Mhe. Elias John Kwandikwa, Mb. Vilevile niwashukuru Katibu Mkuu wa Sekta ya Uchukuzi Eng. Dkt. Leonard Chamurio na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Rashid A. Tamatamah na watendaji wote wa Wizara hizi kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika vikao na kutoa maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati kuchambua Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa ushirikiano

na mchango wa mawazo wakati wote wa kutekeleza kazi hii hadi kuiwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu. Kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge.

1. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb – **Mwenyekiti**
2. Mhe Hawa Mchafu Chakoma, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Eng. Ramo Matala Makani, Mb – Mjumbe
4. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mb “
5. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb “
6. Mhe. Joyce John Mukya, Mb “
7. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb “
8. Mhe. Susan Chogisasi Mgonukulima, Mb “
9. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb “
- 10.Mhe. Nuru Awadh Bafadhili, Mb “
- 11.Mhe. James Francis Mbatia, Mb “
- 12.Mhe. Saul Henry Amon, Mb “
- 13.Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb “
- 14.Mhe. Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb “
15. Mhe. Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mb “
- 16.Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb “
- 17.Mhe. Dua William Nkurua, Mb “
- 18.Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb “
- 19.Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga, Mb “
- 20.Mhe. Rukia Kassim Ahmed, Mb “
- 21.Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb “
- 22.Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb “
- 23.Mhe. Munde Abdallah Tambwe, Mb “
24. Mhe. Abdulazizi Mohamed Abood, Mb “
- 25 . Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb “

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Steven Kagaigai; Kaimu Mkurugenzi wa Kamati Ndg. Michael Chikokoto; Makatibu wa kamati Ndg. Hosiana John Mvunta na Ndg. Janeth Malangu; Mshauri wa Bunge masuala ya Sheria Ndg. Stephano Mbutu pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Modesta Kipiko kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili.

Moshi Selemani Kakoso
MWENYEKITI
KAMATI YA MIUNDOMBINU
21 Mei, 2020

SPIKA: Ahsante sana. Nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Suzan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo na Utoaji Vyeti kwa Wafanyakazi wa Vyombo vya Uvuvi wa Mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6) (c), naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo na Utoaji Vyeti kwa Wafanyakazi wa Vyombo vya Uvuvi wa Mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maoni haya, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliye chimbuko la uhai wa viumbe vyote kwa kunijalia uhai na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kuwasilisha maoni ya Upinzani kuhusu Azimio lililopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado tupo katikati ya janga hili la *Corona* napenda kutumia fursa hii pia kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwakumbusha wananchi wote kuwa janga hili bado lipo, hivyo waendeleo kuchukua tahadhari zote za kujikinga kama inavyoelekezwa na wataalam wa afya. Aidha, Kambi Rasmi

ya Upinzani Bungeni inaendelea kuwafaraji, kuwatia moyo na kuwaombea wale wote waliopata athari za moja kwa moja na Covid 19 kwa kuugua wao wenyewe, kuuguliwa au kufiwa na wapendwa wao. Ee, Mwenyezi Mungu uwaponye na pia kuwapa pumziko la milele wale wote walioaga dunia kwa janga hili popote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nijielekeze kwenye hoja iliyoletwa na Serikali ya kuliomba Bunge liazimie kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo na Utoaji wa Vyeti vya Wafanyakazi wa Vyombo vya Uvuvi wa Mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla kuhusu azimio; Azimio hili linatufunza jambo moja kubwa sana kwamba Tanzania siyo kisiwa; na kwa kuwa Tanzania siyo kisiwa ni lazima iendane na mfumo wa dunia na mifumo mingine changamano ya Kimataifa ili iweze kuendelea kuwepo katika dunia na utandawazi wa ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kadhaa Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikieleza katika hotuba zake kuwa mahusiano ya Kimataifa kupitia mikataba na itifaki mbalimbali ni jambo lenye afya kwa ustawi wa Mataifa husika kama ilivyo muhimu kwa viumbe hai kutegemeana kupitia Ikolojia ili viweze kuendelea kuishi. Pamoja na kwamba sisi ni Taifa huru lenye mamlaka kamili, lakini uhuru huo hauna maana kwamba tunajua kila kitu au kutengeneza kila kitu. Yapo mambo ambayo ni lazima kushirikiana na Mataifa mengine ili tuweze kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi mkataba huu ambao Bunge linaombwa kuiridhia, una maudhui mazuri kwa kuwa utawafanya wananchi wetu ambao ni wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi kuwa na viwango vya Kimataifa na hivyo kuwa na ushindani katika Soko la Ajira la Kimataifa. Aidha, Kifungu cha 9 cha Mkataba huu kinatoa fursa kwa nchi wanachama kuomba kupatiwa msaada wa kitaalam kutoka Shirika la Bahari Duniani kuhusu masuala kadhaa na misingi kama vile:-

- (i) Mafunzo ya wafanyakazi katika ngazi ya uongozi na utaalam;
- (ii) Kuanzisha vyuo vya mafunzo ya wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi;
- (iii) Kutoa vifaa na nyenzo nyingine za ufundishaji katika vyuo vya mafunzo;
- (iv) Uandaaji wa programu za mafunzo za kutosha ikiwa ni pamoja na mafunzo kwa vitendo juu ya vyombo vya uvuvi baharini;
- (v) Kusaidia mbinu na mikakati mingine kwa ajili ya kukuza weledi, ufanisi wa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi hasa kwa misingi ya Kitaifa na Kikanda kwa ajili ya kufikia malengo ya mikataba na kwa kutilia maanani mitaji maalum ya nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na fursa hizo, yapo mambo kadhaa ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuyazingatia. Mambo hayo ni kama yafuatayo:-

- (i) Kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeridhia mikataba na itifaki nyingi za Kimataifa. Hata hivyo, Serikali imekuwa haitekelezi mikataba hiyo kutokana na kukosekana kwa sheria za ndani ili kutoa mwongozo wa utekelezaji wa mikataba husika. Jambo hili halina afya kwa mahusiano yetu Kimataifa na pia halina afya kwa ustawi wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu kuwepo uwajibikaji wa ndani kwa kushindwa kufuata masharti na mikataba ya Kimataifa ni kuwadhulumu wananchi ambao wanalindwa na mikataba hiyo. Kwa hiyo, ili tuweze kuwa sehemu yenye tija katika Jumuiya ya Kimataifa katika jambo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

inashauri na kupendekeza kwamba Serikali ilete haraka iwezekanavyo Muswada wa Sheria ya kusimamia utekelezaji wa mkataba huu kama Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukamataji wa udhibiti wa Vyombo vya Uvuvi vilivyokiuka masharti ya Mkataba. Kifungu cha 8 cha Mkataba huu kinatoa masharti kwamba chombo cha uvuvi cha nchi mwanachama wa Mkataba huu kitakapokuwa kwenye bahari ya nchi mwanachama mwingine, basi kitakuwa chini ya ukaguzi na udhibiti wa Maafisa wa Mamlaka za nchi hiyo ili kuthibitisha kama wafanyakazi wa chombo hicho wamekidhi viwango vya mafunzo vilivyoinishwa na Mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kinaendelea kueleza kwamba ikiwa wafanyakazi watagundulika hawajakidhi vigezo vya mkataba huu na ikionekana kuendelea kwao kufanya kazi kunaweza kusababisha madhara kwa watumia mali na mazingira, basi watachukua hatua za kukishikilia chombo hicho na kuhakikisha kwamba hakiendi kokote mpaka masharti ya vigezo vinavyowekwa na Mkataba huu vinapotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kimetoa masharti kwamba ikiwa chombo kitakamatwa kutokana na kutokidhi masharti ya mkataba huu, basi ukamataji huu basi ukamataji ni lazima ufanyike kwa namna ambayo hautaathiri chombo au kusababisha ucheleweshaji usio wa lazima. Ikiwa ukamataji utafanyika kiholela na kukishikilia chombo bila sababu za msingi, basi mkamataji atatakiwa kulipa fidia ya hasara kwa upotevu wa uharibifu wowote utakaotokana na ukamataji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefanya rejea ya kifungu hicho ili kutoa angalizo kuwa Maafisa au mamlaka zinazokuwa na jukumu la kukamata kuwa makini wasije wakaiingiza nchi kwenye hasara ya kulipa fidia kutokana na ukamataji wa kizembe. Kumekuwa na desturi ya kamata kamata ya kiholela kwa

ajili tu ya kujipatia umaarufu kwenye vyombo vya habari, lakini mwishowe tunashindwa kesi nyingi na kulazimika kulipa mamilioni ya shilingi kama fidia jambo ambalo linaisababishia nchi hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefanya rejea ya kifungu hicho ili kutoa angalizo kuwa Maafisa au Mamlaka zinazokuwa na jukumu la kukamata kuwa makini wasije wakalingiza nchi kwenye hasara na kulipa fidia kutokana na ukamataji wa kizembe. Kumekuwa na desturi hiyo...

NAIBU SPIKA: Nenda namba 15 Mheshimiwa, kama na kwako inasomeka kama niliyo nayo yapa.

MHE. SUSAN L. KIWANGA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: *Okay!*

NAIBU SPIKA: Tafuta inaposema, kumi na tano.

MHE. SUSAN L. KIWANGA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ehee, karibu.

MHE. SUSAN L. KIWANGA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mfano hai wa Meli ya Uvuvi iliyokamatwa na Samaki aina ya Johari maarufu kama ya Magufuli. Meli iliozea baharini na samaki wakataifishwa lakini matokeo yake tulishindwa kwenye ile kesi Na kulazimika kulipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kiwe fundisho na ndiyo maana tunasisitiza itungwe sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mkataba huo ili kusiwe na ukamataji holela. Sheria itamke bayana ikiwa Afisa au Mamlaka iliyopewa

jukumu la kukamata, itakamata kizembe na kusababishia Serikali hasara ya kulipa fidia, basi mkamataji huyo au Mamlaka hiyo iwajibishwe kutokana na uzembe huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha, Mkataba huu utukumbushe kuwa sisi kama Taifa ni sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa na kwa sababu hiyo ni lazima tushiriki na tufuate mifumo ya Kimataifa ili tuweze kuendelea kuwepo katika dunia ya utandawazi. Ili tuweze kuwa kweli sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa, lazima kuwe na dhamira ya dhiti na utashi wa kisiasa katika kutekeleza kikamilifu Mikataba na itifaki mbalimbali za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mikataba na Itifaki hizo ni kilelezo cha dhamira njema na ustawi wa kisiasa cha utekelezaji wa Mikataba na Itifaki hizo. Aidha, utungaji wa sheria hiyo, utasaidia kutoa mwongozo wa utendaji na hivyo kuliepusha Taifa na hasara itokanayo na ulipaji fidia kwa makosa ya uzembe kama vile ukamataji holela wa vyombo vya uvuvi kutokana na kufanya kazi kwa mazoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU
AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA KIMATAIFA WA
VIWANGO VYA MAFUNZO NA UTOAJI VYETI KWA
WAFANYAKAZI WA VYOMBO VYA UVUVI WA MWAKA 1995
(INTERNATIONAL CONVENTION ON STANDARDS OF
TRAINING, CERTIFICATION AND WATCHKEEPING FOR FISHING
VESSEL PERSONNEL, 1995) - KAMA ILIVYOWASILISHWA
MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika,Kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6) (c), naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa

Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo na Utoaji Vyeti kwa Wafanyakazi wa Vyombo vya vya Uvuvi wa Mwaka 1995.

2. Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maoni hayo, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliye chimbuko la uhai wa viumbe vyote; kwa kunijalia uhai na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili, kuwasilisha maoni ya Upinzani kuhusu Azimio lilipo mbele yetu.

3. Mheshimiwa Spika,Kwa kuwa bado tupo katikati ya janga la Corona, napenda kutumia fursa hii pia kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuwakumbusha wananchi wote kwamba; janga hili bado lipo, hivyo waendeleo kuchukua tahadhari zote za kujikinga, kama inavyoelekezwa na wataalam wa afya. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuwafaraji, kuwatia moyo na kuwaombea wale wote waliopata athari za moja kwa moja za COVID -19, kwa kuugua wao wenyewe, kuuguliwa na au kufiwa na wapendwa wao; ili Mwenyezi Mungu awaponye na pia kuwapa pumziko la milele wale wote walioaga dunia kwa janga hili popote duniani.

4. Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nijielekeze kwenye hoja iliyoletwa na Serikali ya Kuliomba Bunge liazimie kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo na Utoaji wa Vyeti kwa Wafanyakazi wa Vyombo vya Uvuvi wa Mwaka 1995.

B. MAONI YA JUMLA KUHUSU AZIMIO

5. Mheshimiwa Spika, Azimio hili linatufunza jambo moja kubwa sana; Kwamba; Tanzania sio kisiwa. Na kwa kuwa Tanzania sio kisiwa; ni lazima iendane mfumo wa dunia (*The World Order*) na mifumo mingine changamano ya kimataifa (*Global Intergrated Systems*) ili iweze kuendelea kuwepo katika dunia ya utandawazi na ushindani.

6. Mheshimiwa Spika, mara kadhaa Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikieleza katika hotuba zake kuwa, mahusiano ya kimataifa kupitia mikataba na itifaki mbalimbali ni jambo

lenye afya kwa usitawi wa mataifa husika kama ilivyo muhimu kwa viumbe hai kutegemeana kupitia Ikolojia (Symbiosis) ili viweze kuendelea kuishi.

7. Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba sisi ni Taifa huru lenye mamlaka kamili (Sovereign State); lakini uhuru huo hauna maana kwamba tunajua kila kitu au tunaweza kila kitu. Yapo mambo ambayo ni lazima kushirikiana na mataifa mengine ili tuweze kuwa bora zaidi.

8. Mheshimiwa Spika, kimsingi Mkataba huu ambao Bunge linaombwa kuuridhia una maudhui mazuri kwa kuwa utawafanya wananchi wetu ambao ni wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi, kuwa na viwango vya kimataifa na hivyo kuwa na ushindani katika soko la ajira la kimataifa. Aidha kifungu cha tisa (9) cha Mkataba huu kinatoa fursa kwa nchi wanachama kuomba kupatiwa msaada wa kitaalam (technical assistance) kutoka Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organization – IMO) kuhusu masuala kadhaa ya msingi kama vile:-

i. Mafunzo ya wafanya kazi katika ngazi ya uongozi na utaalam

ii. Kuanzisha vyuo vya mafunzo ya wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi

iii. Kutoa vifaa na nyenzo nyingine za ufundishaji katika vyuo vya mafunzo.

iv. Uandaaji wa Programu za Mafunzo za kutosha ikiwa ni pamoja na Mafunzo kwa Vitendo juu ya Vyombo vya Uvuvi Baharini

v. Kusaidia mbinu na mikakati mingine kwa ajili ya kukuza weledina ufanisi wa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi; hasa kwa misingi ya kitaifa na kikanda kwa ajili ya kufikia malengo ya Mkataba; na kwa kutilia maanani ya mahitaji maalum ya nchi zinazoendelea.

9. Mheshimiwa Spika, pamoja na fursa hizo; yapo mambo kadhaa ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuyazingatia:- Mambo hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Kuleta Bungeni Muswada waSheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mkataba.

10. Mheshimiwa Spika, Tanzania imeridhia mikataba na itifaki nyingi za kimataifa. Hata hivyo, Serikali imekuwa haitekelezi mikataba hiyo kutokana na kukosekana kwa sheria za ndani ili kutoa mwongozo wa utekelezaji wa mikataba husika. Jambo hilo halina afya kwa mahusiano yetu kimataifa na pia halina afya kwa ustawi wetu wa ndani. Nasema hivi kwa sababu; kukwepa uwajibikaji wa ndani kwa kushindwa kufuata masharti ya mikataba ya kimataifa ni kuwadhulumu wananchi ambao wanalindwa na mikataba hiyo. Kwa hiyo, ili tuweze kuwa sehemu yenye tija katika Jumuiya ya Kimataifa katika jambo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba; Serikali ilete haraka iwezekanavyo Muswada wa Sheria ya Kusimamia utekelezaji wa makataba huu kama Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyoelekeza.

ii. Ukamataji na Udhibiti wa Vyombo vya Uvuvi vilivyokiuka Masharti ya Mkataba

11. Mheshimiwa Spika, kifungu cha nane (8) cha Mkataba huu kinatoa masharti kwamba Chombo cha Uvuvi cha nchi mwanachama wa mkataba huu kitakapokuwa kwenye Bandari ya nchi mwanachama mwingine; basi kitakuwa chini ya ukaguzi na udhibiti wa maafisa wa mamlaka za nchi hiyo ili kuthibitisha kama wafanyakazi wa chombo hicho wamekidhi viwango vya mafuzo vilivyoanishwa na Mkataba huu.

12. Mheshimwa Spika, kifungu hiki kinaendelea kueleza kwamba, ikiwa wafanyakazi watagundulika hawajakidhi vigezo vya mkataba huu na ikaonekana kuendelea kwao kufanya kazi kunaweza kusababisha madhara kwa watum mali na mazingira basi watachukua hatua ya kukishikilia

chombo hicho na kuhakikisha kwamba hakiendi kokote mpaka masharti na vigezo vilivyowekwa na Mkataba huu vitakapotekelezwa. Unduly detained.

13. Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kimetoa masharti kwamba ikiwa chombo kitakamatwa kutokana na kutokidhi masharti ya mkataba huu, basi ukamataji huo lazima ufanyike kwa namna ambayo hautaathiri chombo na au kusababisha ucheleweshaji usio wa lazima. Ikiwa ukamataji utafanyika kiholela na kukishikilia chombo bila sababu za msingi basi mkamataji atatakiwa kulipa fidia ya hasara kwa upotevu au uharibifu wowote unaotokana na ukamataji huo.

14. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefanya rejea ya kifungu hicho ili kutoa angalizo kwa maafisa au mamlaka zitakazokuwa na jukumu la kukamata kuwa makini wasije wakaiingiza nchi kwenye hasara ya kulipa fidia kutokana na ukamataji wa kizembe! Kumekuwa na desturi ya kamata kamata ya kiholela kwa ajili tu ya kujipatia umaarufu kwenye vyombo vya habari lakini mwishowe tunashindwa kesi nyingi na kulazimika kulipa mamilioni ya shilingi kama fidia jambo ambalo linaisababishia nchi hasara kubwa.

15. Mheshimiwa Spika, Tuna mfano hai wa Meli ya Uvuvi iliyokamatwa na Samaki aina ya jodari maarufu kama Meli ya Magufuli; Meli iliozea baharini na samaki wakataifishwa lakini matokeo yake tulishindwa kwenye ile kesi na kulazimika kulipa fidia. Kifungu hiki kiwe fundisho na ndio maana tunasisitiza itungwe sheria ya kusimamia utekelezaji wa mkataba huu ili kusiwe na ukamataji holela. Na sheria itamke bayana ikiwa afisa au mamlaka iliyopewa jukumu la kukamata, itakamata kizembe, na kuisababishia Serikali hasara ya kulipa fidia basi mkamataji huyo au mamlaka hiyo iwajibishwe kutokana na uzembe huo.

C. HITIMISHO

16. Mheshimiwa Spika, mkataba huu utukumbushe kuwa sisi kama Taifa ni sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa; na kwa

sababu hiyo, ni lazima tushiriki na tufuate mifumo ya Kimataifa ili tuweze kuendelea kuwepo katika dunia ya utandawazi. Ili tuweze kuwa kweli sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa ni lazima kuwe na dhamira ya dhati na utashi wa kisiasa (political will) katika kutekeleza kikamilifu mikataba na itifaki mbalimbali za kimataifa. Hivyo, kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mikataba na itifaki hizo ni kilelezo cha dhamira njema na utashi wa kisiasa cha utekelezaji wa mikataba na itifaki hizo. Aidha, utungaji wa sheria hiyo, utasaidia kutoa mwongozo wa utendaji, na hivyo kullepusha taifa na hasara itakanayo na ulipaji fidia kwa makosa ya uzembe kama vile ya ukamataji holela wa vyombo vya uvuvi kutokana na kufanya kazi kwa mazoea.

17. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Susan Limbweni Kiwanga (Mb)
**KNY. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI, KATIKA WIZARA YA UJENZI,
UCHUKUZI NA MAWASILIANO**
21 Mei, 2020

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa mawasilisho, ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wangetaka kuchangia kwenye azimio hili. Tutaanza na Mheshimiwa Ally Saleh, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ajiandae.

Mheshimiwa Ally Saleh Msekwa, wataalam wetu Mheshimiwa Ally Saleh hatumsikii huku kwenye ukumbi wa Bunge. Tutarudi Msekwa sauti ikiwa imesharudi Mheshimiwa Injinia Ramo Makani atafuatiliwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ajiandae.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa. Nimshukuru Mwenyezi Mungu

kwa afya jambo ambalo limeniwezesha kusimama mbele ya Bunge Tukufu ili kutoa mchango wa maoni kwa ajili ya hoja iliyoko mbele yetu ambayo kimsingi ni kuendelea kushauri Bunge liweze kuridhia azimio hili muhimu sana kwa Taifa letu. Kwa kuwa hili ni azimio la mwaka 1995 mwaka ambapo lilitiwa saina, inawezekana wengine wakaona kwamba tumechelewa sana kufanya mchakato huu wa kuridhia, lakini niwatoe mashaka tu kwamba hata lilipotiwa saina mwaka 1995 utekelezaji wake ulikuja kuanza mwaka 2012 kwa mara ya kwanza kabisa, ukihesabu hiyo kama ni miaka 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha kwamba, hata Kimataifa nchi zote duniani zilichukua muda kutekeleza kwa sababu mbalimbali ambazo nyingi ni za kiufundi. Kwa hiyo na sisi hatujachelewa tuko vizuri. Kwa hiyo niipongeze Serikali kwa kuleta azimio hili mbele yetu, pia kwa kuleta kwa wakati kwa sababu mtakumbuka tumepitisha Sheria jana inayohusu uvuvi kwenye Bahari Kuu. Kwa kweli kama ingekuwa azimio hili bado halijaletwa changamoto zingekuwa nyingi sana kwenye eneo hilo kwa sababu sisi tungekuwa hatumo ndani ya shughuli hiyo muhimu inayofanyika Kimataifa na kutokuwemo kwetu ni kutokuwemo kwenye mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa sasa niipongeze Serikali kwanza kwa kuleta mkataba huu mbele ya Bunge, pia nipongeze Bunge kwanza kwa kupokea na kukubali kujadili, pia sasa hivi Bunge likubali sasa hayo ni maoni yangu, kuridhia mkataba huu muhimu. Kwa kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati inayohusika na tumechakata kwa kiwango kirefu nikubaliane na maoni yote yale ambayo tumeyatoa kupitia taarifa ya Kamati. Kwa kuwa taarifa imesomwa mbele ya Bunge basi nisirudie tena yaleyale ambayo Kamati yangu imewasilisha mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msisitizo tu kidogo nizungumzie jambo moja ambalo mchangiaji aliyetangulia kati ya wachangiaji wa mwanzo, mimi ni mchangiaji wa kwanza kwa maana ya kuchangia, lakini taarifa zimesomwa, iko taarifa ya kutoka ndugu zetu wa upande wa upinzani, ni

mashaka kidogo tu wanayo yanayohusiana na utekelezaji, baada ya kutia saini makubaliano haya mkataba huu wana mashaka kwamba kwenye utekelezaji kunaweza kujitokeza changamoto za utekelezaji mbaya au mbovu, yametumika maneno ya kamatakamata kwamba tunaweza tukafanya kamatakamata kwenye vyombo vya Kimataifa kule na pengine ulitolewa hata mfano wa matukio ya nyuma kwamba tunaweza tukaingia kwenye matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba ndiyo maana mkataba huu unatupeleka mahali ambapo tunakwenda kuwa makini zaidi kwenye kupata wataalam katika ngazi ya *training*; kutoa mafunzo na kutoa vyeti. Unajua kuna ngazi hizo mbili; kwanza unajiimarisha kwenye kutoa mafunzo kwa maana hapo unazungumzia *academic training*, lakini baada ya hatua ile utafika kwenye hatua *professionalism* ambako sasa kule nako na nchi yetu iko vizuri tu, tunacho chombo kinachoratibu ile taaluma yenyewe, baada ya kuwa mtu amepata mafunzo sasa kwenye utekelezaji wa kazi anakwenda kuratibiwa huko.

Kwa hiyo baada ya kuwa na wataalam hao makini, ambapo sasa tunaeeleka huko baada ya kuwa tutazingatia sana masharti ya mkataba huu, basi tutakuwa tuko vizuri na kwa hiyo hakuna wasiwasi wa kutokea kwa mashaka yale yanayozungumziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipengele kilizungumzwa na hii ni hoja ya Kamati pia nami nisisitize tu kwamba, mkataba huu umeandikwa katika lugha sita za Kimataifa na sisi kama Kamati tumesema kwamba Serikali sasa ifuate taratibu zinazostahiki ili tuweze kuingiza Kiswahili, kutoa mapendekezo kwa maana Kiswahili nacho kiingie kwa sababu imegundulika katika utafiti mbalimbali Kimataifa kwamba kwenye hizi jumuiya mbalimbali za Kimataifa unavyozidi kuwa na lugha nyingi zaidi zinazotumika kwenye uandishi wa nyaraka, kwenye mijadala, kwenye mikutano na mahali pengine, kunapokuwa kumetumika lugha nyingi zaidi, basi kasi ya utekelezaji wa hayo yanayohusika kwenye huo mkusanyiko inakuwa ni kubwa na nzuri na yenye tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nisisitize pia kwamba lugha ya Kiswahili na yenyewe iweze kwenda kuorodheshwa iwe sasa ni lugha ya saba isichelewe ikaingia nyingine kabla ya hii ya kwetu, basi baada ya kuwa ziko sita na lugha ya Kiswahili iingie kama lugha ya saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya kupata wataalam wetu wenyewe ambao watakuwa mahiri ni pale ambapo tunaenda kuunganika na wenzetu ambao tayari wako kwenye hatua kubwa zaidi ya ujuzi katika eneo hili la vyombo vya uvuvi. Tuna vyo vitano vimetajwa kile cha Bagamoyo, kule Pwani; Nyegezi kule Mwanza; Kibirizi, Kigoma; Rorya, Mara; na Mikindani kule Mtwara. Wenyeji kwenye maeneo haya haina maana ya kwamba ni wenyeji tu peke yake, lakini kwa umuhimu wa kwanza kwa sababu walioko karibu wanaweza kupata uwezekano zaidi wa kuhudhuria kwenye vyo hivyo kwa uwingi zaidi, basi wenyeji kwenye maeneo haya wanaenda kupata faida, kwa sababu wakipata sifa za Kimataifa basi maana yake wanakuwa kwenye viwango vya kuweza kuajirika kwenye nchi zingine ambako wanaweza kupata kazi kwenye mashirika mengine duniani.

Pia na sisi kwa kuwa na idadi ya wataalam wengi ambao watakuwa wamefundishwa vizuri na wamepata vyeti vinavyostahili na vinavyokubalika duniani maana yake ni kwamba hata tunapokwenda kufanya usimamizi sasa ule wa shughuli zote za uvuvi wa bahari kuu pamoja na usimamizi wa mazingira na kadhalika, basi ule ukaguzi wetu na usimamizi wetu utakubalika kwa sababu vinginevyo unawezaje kumkagua mtu ambaye yeye anajua wewe huna sifa za kumkagua, hutaweza. Sasa sisi katika hatua hii kwa kuwa tunakwenda kuwa na sifa hizo ambazo zitakuwa zinatambulika duniani, basi tunakwenda kustahili hata kwenda kuwasimamia wale watakaokuja kufanya shughuli kama hizo za uvuvi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema pale mwanzo kwa kiwango kikubwa maoni yaliyotolewa kwenye taarifa ya Kamati, mimi ni sehemu yake. Baada ya haya, naunga mkono hoja mkataba huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua na Mheshimiwa Mbaraka Dau ajiandae.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia azimio lililo mbele yetu. Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu ambaye ametufikisha siku ya leo tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua wasaa huu kuipongeza Serikali kwa namna ilivyoona umuhimu na uharaka wa kuleta azimio hili mbele ya Bunge lako Tukufu ili tuweze kuliridhia kama ambavyo nchi nyingine za Afrika ama huko duniani ambapo tayari wameshaliridhia azimio hili. Kama ambavyo ilivyowasilishwa na Kamati ya Kudumu ya Miundombinu, umuhimu na faida nyingi za azimio hili ambapo kimsingi mapendekezo na ushauri tunaishauri Serikali kuona namna bora ya kulifanyia haraka suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza napenda sana kuishauri Serikali, kulichukulia suala hili kwa mapana makubwa na kimsingi hii ina faida kubwa kwa wavuvi wetu, kwa sababu wavuvi wetu watapata sasa ile hadhi ya kimataifa ya kuweza kuajirika katika nchi yoyote duniani, *so far* watakuwa wana ile *certificate*. Kwa hiyo ile inakuwa kama kiingilio ama ile inakuwa kama ni *document* inayowawezesha kufanya kazi nchi yoyote duniani. Kimsingi tunafahamu faida za kufanya kazi Kimataifa, hizi zinaenda kuongezea ama zinaenda kupelekea ongezeko la fedha za kigeni ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, binafsi niendeleo kuipongeza sana Serikali kwa namna ilivyoleta azimio mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine, tunapenda sana kuishauri Serikali, sasa kama tayari tunaenda kuridhia azimio hili ione sasa umuhimu wa kufanyia kazi Sera ya Uvuvi ili iweze kuendana sambamba na hali ama na azimio hili jinsi namna linavyotaka. Sambamba na uandaaji wa sera, lakini pia iangalie sheria ambazo kwa

namna moja ama nyingine *either* zitaweza kwenda kukinzana na sheria mbalimbali ama zitakazoenda kukinzana na azimio hili ili ziweze kwenda kusoma sambamba ama ziweze kuwezesha wavuvi wetu pamoja na hawa wenye vyombo vya uvuvi kwenda kufanya kazi inayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni pendekezo la Kamati, lakini napenda kulisisitiza kuhusiana na namna ya kuona lugha ya Kiswahili iweze kuingia. Ibara ya 12 kama sijakosea inatoa mwanya kwa nchi mwanachama kuweza kupeleka mapendekezo ama kuweza kuweka nyongeza katika azimio hili. Kwa hivyo tunapenda kuishauri ama kuitaka Serikali itumie nafasi hiyo kuweza kuandaa pendekezo la kupeleka mapendekezo hayo *IMO* kuona ni namna gani lugha ya Kiswahili na yenyewe inakuwa miongoni mwa lugha saba ambazo zitakuwa zinatumiwa katika azimio hili. Pia mara kadhaa tumemsikia Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akisisitiza umuhimu wa lugha ya Kiswahili na vile vile tunaweza tukaona utajiri uliopo katika lugha hii ya Kiswahili unajitosheleza kabisa kuingia na kuwa lugha ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona faida zitakazopatikana endapo tutapitisha azimio hili ikiwemo kuimarika kwa upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali katika Sekta ya Uvuvi. Kama tunavyofahamu unapokuwa na takwimu, unapokuwa na namba, unapokuwa na taarifa, unaweza kufanya maamuzi yaliyokuwa sahihi kabisa. Kwa maana hiyo tunaipongeza sana Serikali kwa namna ya kipekee ilivyoona itulettee azimio hili ndani ya Bunge lako tukufu ili tuweze kulipitisha.

Mbali ya upatikanaji wa takwimu pamoja na taarifa sahihi, pia umuhimu na faida wa azimio hili linatupelekea kuimarisha usalama wa wafanyakazi katika vyombo vya uvuvi na hivyo kupunguza ajali. Kwa maana hiyo itasaidia vyombo vya uvuvi na wavuvi wetu watakuwa katika mikono sahihi ama mikono salama ya kuweza kupata usalama watakapokuwa wanaendelea na jukumu zima la ufanyaji wa kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo pia niendeleo kuipongeza Serikali ilivyoona umuhimu wa kutuletea hili azimio kwa wakati kabisa na kwa maneno mengine niseme wakati mwingine tulichelewa kabisa katika kulipitisha hili azimio.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na pengine nitumie nafasi hii kuwashukuru Katibu wa Bunge na Makatibu wetu wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kwa namna tulivyoweza kulichakata azimio hili na kuonyesha umuhimu wake kwa nchi yetu, pia umuhimu kwa Serikali yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mheshimiwa Ally Saleh ajiandae.

MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya mimi kutoa maoni yangu kuhusiana na mkataba uliopo mbele yetu, ambao kimsingi ninayo kila sababu ya kuanza kuipongeza Serikali kwa kuleta mkataba huu ili uweze kuridhiwa na Bunge, hatimaye uweze kuanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuifanya sekta isimamiwe katika sura ya Kimataifa kuna maana sana katika kuifanya sekta hiyo ikue, lakini kuna maana sana katika kuimarisha usimamizi katika sura hiyo ya Kimataifa, Tanzania ni nchi yenye utajiri mkubwa wa bahari, karibu mashariki mwa nchi yetu kote kuna bahari ya hindi ambayo kimsingi inaonekana wazi bado tupo kwenye mchakato wa kuwekeza kwenye sekta hii. Zipo nchi duniani zinaendesha uchumi wake kwa kutegemea bahari peke yake; hii ina maana kwamba kadri tunavyoendelea kutengeneza miongozo, sheria iliyopitishwa katika Bunge hili hivi karibuni pamoja na kuridhia azimio hili kwa ajili ya kulipitisha lianze kufanya kazi, kuna maana sana katika kuimarisha sekta hii ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama umesikia hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani inaonyesha pia faida kubwa ya kuridhiwa kwa mkataba huu. Hii ina maana kwamba hatuna sababu ya kuacha kuridhia. Mambo ya nyongeza yamezungumzwa kama vile kuhakikisha kwamba tunatumia lugha ya Kiswahili kama miongoni mwa lugha zitakazotumika kuandaa mkataba huu pamoja na kuwepo kwa sera ya bahari; haya ni mambo ya msingi katika kuhakikisha kwamba mkataba huu unakuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yapo masuala mengine ya msingi ambayo katika kujipanga tunapotaka kupitisha mkataba huu ni muhimu Serikali iyaone. Moja ya mambo hayo ni kuwepo kwa chombo maalum kinachosimamia Sekta ya Uvuvi, nadhani hili ni jambo la msingi sana. Tuna sekta mbalimbali zinasimamiwa na mashirika, lakini nadhani kuna pengo katika Sekta ya Uvuvi ili iweze kuwa sekta inayochangia kwa kiwango kikubwa sana na kwa ufanisi katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, lakini naona ipo sababu sasa ya Serikali kuwekeza kwenye uvuvi huu wa bahari kuu na kuwekeza kwenyewe kunaweza kwenda sambamba na kununua meli kubwa za uvuvi kama ambavyo tuna meli zinazofanya kazi kwenye maziwa makuu yanayozunguka nchi yetu, tunapaswa pia kuwa na meli kwa ajili ya kushiriki kwenye shughuli za uvuvi wa bahari kuu ili kuendelea kupata kipato kikubwa kinachotokana na utajiri ulipo kwenye bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, mimi niseme ni Mjumbe wa Kamati na nakubaliana kwa dhati kabisa na nia hii ya Serikali ya kuleta azimio hili na nawaomba Waheshimiwa tuliridhie ili Serikali iweze kutekeleza majukumu yake na wavuvi pamoja na watu wanaofanya kazi kwenye sekta waweze kutambulika katika sura ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mbaraka Dau atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh na Mheshimiwa Rukia Kassim ajiandae.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye azimio hili muhimu sana. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa na kufanya masuala yanayohusu nchi yetu. Nianze kwa kusema kwamba naunga mkono azimio hili la Bunge kuridhia itifaki hii, lakini jambo la pili ni jana tu hapa tumepitisha Sheria muhimu sana ya Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu. Sasa ujio wa itifaki hii ya kuridhia azimio hili imekwenda vizuri kabisa na sheria ile tuliyoipitisha jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ujio wa itifaki hii ya kuridhia Azimio hili ime-*consider* vizuri kabisa na sheria ile ya jana. Yamesemwa mengi lakini naomba nichangie kidogo kuhusu suala la ajira. Vijana wetu watapata ajira, na katika moja ya matatizo ya sheria ambayo ilifutwa jana ile iliyoleta Mamlaka ya usimamizi wa *DSFA* ilikuwa ni kwamba. Kulikuwa na kanuni na Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi anafahamu, kulikuwa na kanuni inayotaka kwamba meli zinazokuja kuvua katika *EEZ* yetu, zichukue Mabaharia wa Kitanzania na kanuni hiyo ilikuwepo katika sheria tuliyoifuta jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ilikuwa kama tunalazimisha kwasababu Mabaharia wa Tanzania walikuwa hawana sifa hizi ambazo leo itifaki hii sasa inaenda kuwapa Mabaharia wa Tanzania. Kwasababu Vyuvo vyetu vile cha Mbegani, Nyegezi kule Mikindani pamoja na Rorya na kule Kibilizi, vilikuwa uwezo wao mwisho wa meli zenye urefu wa mita 23 tu. Kuanzia 24 na kuendelea tulikuwa hatuna uwezo huo wa kuwafundisha Mabaharia wetu. Sasa kwa kuazimia kwa kukubali Itifaki hii, maana yake kwamba sasa Mabaria wetu wataweza kukubalika Kimataifa na wataweza sasa kwenda kwenye zile Meli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *EEZ* yetu na jana nilisema hapa, kule tuna *square kilometer* zaidi ya laki mbili

na meli zinazokuja kuvua kule kwa wakati mmoja zinaweza zikafika mpaka meli 100. Sasa ushauri wangu na baadae nitatoa na ushauri mwingine. Lakini nianze kwa kusema ushauri huu muhimu kabisa, Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi, pamoja na Waziri wa Uchukuzi, Mawasiliano na Ujenzi. Mkae pamoja msaidiane katika kutengeneza zile kanuni na sheria tumeipitisha jana ili Mabaria wetu sasa. Kwa mfano labda kila meli inayoingia katika *EEZ* yetu labda kuwe na Mabaharia watatu au wanne au watano kwa meli 100 ambazo zinafanya kazi kule kwenye *EEZ* tunaweza tukajikuta tuna vijana kama labda 500, 1000 wanapata ajira kule kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini limezungumzwa hapa suala la *fishing observers* na hili nalo pia lilikuwepo kwenye kanuni ya sheria tuliyoifuta jana. Kwamba *fishing observer's* ambao wanatakiwa waingie katika meli zile zinazokuja kuvua katika *EEZ* yetu, waweze kufanya kazi ya *stock verification* na tulikuwa pia tunalazimisha hiyo kanuni. Kwamba hawa waende lakini kiukweli hasa, sifa *fishing observers* wetu walikuwa hawana kwa sababu Vyuvo vyetu vilikuwa havina uwezo wa kutoa hivyo vyeti, sasa hili nalo linakwenda kutibiwa, lakini litatusaidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, litatusaidia kwa maana ya kwamba ile utunzaji wa mazingira kuweza kujua *stock* yetu kama meli moja inaweza kuna meli nyingine zina tani mpaka 3000, 2000 sasa zinavua meli 100 unakuta kuna matani malaki kwa malaki. Wanavua halafu wanaondoka, hakuna mtu ambaye ana-*verify* ile *stock*. Sasa hawa *stock observers* watakapokwenda kule wataweza kujua sasa meli fulani imevua labda tani 500 au tani 700 mpaka zitakapoondoka zile meli, mwisho wa siku sisi na Wizara mtakuwa mna uwezo wa kujua sasa kwamba katika msimu huu wa labda wa uvuvi wa Tuna Tanzania wamevuliwa Tuna labda tani laki mbili, laki tatu, laki nne tutaweza pia kuweka mambo yetu sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni suala hili la vyeti, kwamba vyeti vyetu na hili nilishalizingumza vyeti vyetu sasa vitaweza kutambulika kimataifa na suala la usalama. Lakini kubwa zaidi ni ushauri, ushauri ningeomba

sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Vile vyuo vyetu sasa kile cha Mbegani pale Bagamoyo VETA pale, Nyegezi, Mikindani, Rorya, Kibilizi kutokupewa hii sifa ya kuweza kutoa vyeti ni jambo moja. Lakini kutoa vyeti vyenye ubora ni jambo jingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Vyuo lazima viimarishwe viwe na vifaa, viwe na Wataalam tusiishie tu kutoa vyeti mradi vyeti. Kwa sababu katika moja ya mambo ambayo tulikutana nayo tulipokwenda kutembelea pale DSFA Zanzibar wakasema kwamba Mabaharia wetu tulipolazimisha ile kanuni ya Baharia waingie katika zile meli zinazovua katika Bahari Kuu walipelekewa Mabaharia wa Kitanzania 20. Wale wakawachukua, lakini wale wenye meli kufika kule wimbi na misukosuko ya bahari kwasababu Bahari Kuu kule Bahari inakuwa ni *rough* sana. Wale vijana wa Kitanzania walishindwa kufanya kazi wakaishia kulala tu mle kwenye meli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni jambo la msingi sana, tusiishie tu kutoa vyeti. Lakini na vijana wetu wawe competent watakapokwenda kwenye zile meli, wakafanye kazi yenyewe halisi ambayo wanakwenda kuifanya. Kwa hiyo, wanatakiwa wapikwe kisawa sawa, pamoja na hili la vifaa vya ufundishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine nimelizungumza lakini katika namna tu ya kusisitiza. Kwenye utungaji sasa wa Kanuni, Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi kanuni zako lazima sasa zitoe upendeleo kwa Watanzania kwamba katika EEZ wakija kuvua basi meli moja labda iwe na Watanzania watano, sita hata kumi ili vijana wetu sasa waweze kunufaika na hili azimio na tuweze kutoa ajira nyingi sana kwa vijana hawa watakaokwenda kuvua katika Bahari Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu yalikuwa ni hayo na ninaridhia na naunga mkono kama Bunge liridhie Azimio hili. Ninakushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Ally Saleh atafuatiwa na Mheshimiwa Rukia Kassim, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko ajiandae.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia katika siku nyingine kuhusiana na masuala ya mambo ya bahari. Jana tulipitisha sheria ya uvuvi wa Bahari Kuu na ambayo itafika mpaka ita-include mpaka eneo ambalo Zanzibar ipo japokuwa kuna maneno au wengine tunaamini hili si jambo la Muungano na kwa hivyo pengine usimamizi wake uwe makini ili hilo lisilete tatizo kama ambavyo pengine inaweza kutokezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu kupitishwa kwa Itifaki hii ni muhimu sana kwasababu hivi sasa tutakuwa tunaweza kushiriki katika mchakato mzima wa masuala haya ya uvuvi wa Bahari Kuu kwasababu tutakuwa tumeingia katika vigezo na viwango ambavyo vinafanana. Na ndio maana mkataba huu kuna sehemu inasema kwamba nchi sio tu zifike viwango lakini hata iki-exceed viwango ili muweze kufanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitazungumza mambo ya jumla tu kidogo na nitaanzia kwenye suala la lugha ya Kiswahili. Kamati imesema hapa na pengine wasemaji mmoja mmoja kwamba tujaribu na sisi kusukuma Kiswahili ndani ya Itifaki hii. Na Kiswahili kiwemo katika zile lugha ambazo tayari zimetajwa. Hili ni jambo zuri lakini sifikiri kwamba tufanye kwa haraka, kwasababu lazima na sisi tujitayarisha tuwe na Istilahi za kutosha juu ya matumizi ya Kiswahili. *Engine* inaitwa nini, *mtambo* unaitwa nini, *Bycatch* inaitwa nini, mambo yote mengine yanayofanana na hayo ya kiufundi na mengine tutengeneze Istilahi za kutosha ili tuweze kukubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukataka Kiswahili kisitumike na ukatengeneza cheti chako kwa Kiswahili lakini ukakuta inakwenda kwenye meli, kwenye meli mle hakuna mtu yoyote pengine hata Kiingereza hajui. Waliomo mle ndani sio uuze Kiswahili pengine waseme lugha nyingine, kwa

hivyo hili sio suala la ku-*rash* ni kweli tunataka lugha yetu iwe kubwa na tuenee lakini tujitayarisha vizuri tukiingia isiwe kwenda kukwama au kubezwa vyeti vyetu au namna ambavyo sisi wenyewe tunaweza kufanya tukaenda nje. Wataalamu washirikishwe tuweze kuwa na Isilahi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili tunazungumza habari ya sasa kama tukifunua, tukifungua suala hili la uvuvi wa Bahari Kuu na kama tunaingia katika Itifaki hii hivi sasa ina maana kwamba kama wanavyosema watu wengine *at one time* inawezekana ukawa na meli 200, 300 ambazo zinavua katika eneo. Jana mtu mmoja alisema eneo ambalo tunalizungumza linaweza likawa *two hundred thousand square* meters ambalo pengine ni sehemu yetu ambayo ni eneo letu la kujidai

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hilo ni eneo kubwa na ikiwa sera zitakwenda vizuri, sheria zitakwenda vizuri na Bahari bado ni bikra kwa maana kwamba samaki wapo wa kutosha kwa hivyo inawezekana watu wengi wakaja wakataka kuitumia bahari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo ina maana pia idadi ya wataalam wa kila aina wawe wengi. Jana nilizungumzia habari ya kuimarisha Vyuu vyetu, na hapa leo nataka ni-*suggest* kwamba katika hali hii tunayokwenda nayo kuna umuhimu sasa wa kuwa na Chuo Zanzibar pia ambacho kinaweza kikakidhi au kikasaidia sana katika eneo hilo. Zanzibar *by nature* ni watu wa bahari lakini hata ambao sio watu wa bahari wanaweza wakaja wakasoma. Kwa hivyo katika mipango ya maendeleo katika namna ya kutengeneza mazingira ya sheria hii au Itifaki hii ifanye kazi vizuri tufikirie pia kuweka Chuo Zanzibar *strategically* cha Mbegani kiendeleo na vingine viendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unaweza ukasema kwamba Itifaki hii sasa itatuweka sawa kama ambavyo miaka miwili nyuma tulipitisha sheria au tulipitisha Itifaki juu ya Mabaharia. Maana yake ukipitisha Itifaki unakuwa katika kiwango cha Kimataifa. Tulipopitisha Itifaki ile ya Mabaharia

ina maana tuliwatengenezea Mabaharia wetu katika meli za kawaida za kusafiri za mizigo, pengine *tanker*, pengine meli za watalii kuweza kutambuliwa na kuweza kupata haki zao sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ule pengine ilikuwa kama kuna kazi ambayo inaweza ikanipa dola 2000, kwa kuwa sisi tulikuwa sio *signatory* wa mkataba tulikuwa tunaweza tukapunjwa na tunaambiwa kwamba mamilioni ya dola yamepotea kwa wananchi wetu kulipwa kidogo au kupunjwa au kukoseshwa zile haki ambazo Baharia anatakiwa azipate kwa sababu ya kwamba sisi hatukuwa *signatory*.

Mheshimwia Naibu Spika, kwa hivyo Itifaki hii inatuweka sasa watu wetu ambao watakwenda katika hizo meli kukagua au watafanya kazi, watalipwa katika viwango vinavyofanana na wenzao ambao wana elimu na wana uwezo kama ambao wao tunatarajia watakuwa nao. Nasema tunatarajia kwasababu ni sasa mpira uko kwetu baada ya kupitisha Itifaki hii namna gani sasa sisi tutachukua hivyo viwango ambavyo vinatakiwa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba Itifaki inaelezea kwamba kuna maeneo matatu ambayo inayataja ni muhimu. Mojawapo kuhakikisha udhibiti wa Bandari kwa dola, yaani dola iwe na udhibiti wa bandari kwa maana kwamba inahakikisha usalama wa watu wanaokuja, haki zao na kila kitu kiwe sawasawa. La pili wanasema kujenga mfumo wa mawasiliano na Shirika la Maritain la Ulimwengu ni muhimu sana. Na la tatu tunazungumzia juu ya *quality standard system* yaani kila kitu chetu kifanane na wenzetu wengine isije kuwa sisi tuna *below standard* ambayo itatutia hila au itatufanya tusiweze kuonekana kwamba tupo sawa na wenzetu katika hali ya ushindani kwasababu hata kama watu wanavua Bahari Kuu watakapokuja huku Bahari ya Ndani watakapokuja katika Bandari zetu tuwe tunafanana vigezo na watu wengine wa kiulimwengu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine tunazungumzia kwamba tunaweza tukawa na namna ambayo tumekuwa na makubaliano au mipango *at sub or regional level*. Kwa hivyo tujaribu ku-*study* wenzetu ambao wameingia katika mkataba huu ingawa wameanza kazi 2012 tu sisi zamani lakini wako pengine wenzetu wameingia katika eneo hili tujaribu kuona wao wamefanya nini, na tujaribu kufanya nao kazi pamoja ili tuwe na vigezo ambavyo vinafanana na sisi tusitake ku-*reinvent* za *Will* wakati *Will* tayari imeshatengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo kama kuna nchi na kwasababu mkataba unaruhusu kuwa na *sub regionals au regional standards* kwa hivyo hiyo tunaweza tukalifanya. Lakini cha muhimu pia ni kwamba kwa mujibu wa *article* 11 inazungumzia mambo mengine matano mojawapo fursa hii inasaidia katika kufuzu namna ya Uongozi kwasababu unaweza ukaona Bahari au unaweza kuona mafuta. Lakini pia kuna namna ya kujua kuendesha bahari, kuendesha biashara ya bahari au wavuvi bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inasaidia kutoa mafunzo na pia kufadhili Vituo vya Mafunzo. Kwanza ni Utawala lakini pili kwenye Vituo vya Mafunzo ndio hivyo Vyuho ambavyo tumevisema. Lakini inasaidia kuleta *supply of equipment* kwa hivyo sisi tukijipanga tunaukosefu wapi au tuna shida maeneo gani tunaweza sasa fursa ya kutumia kusaidiwa au njia yoyote ile kuweza kupata *equipment*. Jingine ni kuwa na mpango endelevu wa maendeleo wa mafunzo na *equipment* na kila kitu. Kwa hivyo tutafaidika pia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika na la tatu kama nilivyotangulia kusema ni kwamba, inaweza ikatusaidia kuwa na *sub originally approach* ya namna ya sisi tunavyoweza kufanya. Kwa mfano kuna wenzetu pengine Kenya wanatumia Bahari Kuu kuvua na pengine *Mozambique*, itakuwa vizuri kuwa na *standard* ambazo zinafanana miongoni mwetu. Lakini pia wakati huo huo tu kuwa na zile *standard* za Kimataifa.

Mheshimwia Naibu Spika, mie naamini Itifaki hii itakuwa kusaidia sana kuimarisha ile nia yetu ya kutumia uvuvi wa Bahari Kuu na tutapata faida tu ikiwa tutakuwa na viwango kwasababu viwango ndio ambavyo vitapasisha namna ambavyo tunavua namna ambavyo tunatunza mazingira na namna ambavyo kama mtu mmoja alivyosema hapa, hata ile afya au ile hali ya afya ya wafanyakazi na yale mazao ambavyo tunayakusanya yawe ya kimataifa ili yatakapouzwa nje yawe yanaweza kukubalika na isije yakawa-*reject*. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Rukia Kassim atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko. Mheshimiwa Charles Kitwanga ajiandae.

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nami kuweza kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia katika kuridhia Azimio hili ambalo Serikali imetuletea hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na-*declare interest* kama Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu mambo mengi tulishayazungumza katika Kamati na tayari yalishaelezewa hapo kwenye hotuba yetu. Lakini nasema kwamba hatujachelewa, ingawa sisi ni wa 32 katika kuridhia azimio hili lakini nasema kama kutangulia si kufika. Muhimu ni Serikali kujipanga sasa, isiwe kwamba tunaridhia tu, tujipange kwa kujiona kuwa sasa tumeingia katika kuridhia hili ili sasa tuongeze Vyuo na pia tuboreshe Vyuo vyetu ili tuweze kutoa wanafunzi wengi na wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini vijana wetu wana uwezo wa kutosha wa kuweza kusoma na wakapata vyeti ambavyo vitakubalika katika kufanya kazi katika meli hizi za uvuvi wa bahari kuu. Lakini pia Serikali isitake tu kuwa wafanyakazi katika meli za wenzetu kwenye uvuvi huu. Lakini pia Serikali iweze kununua meli ambazo zina uwezo wa kuweza kufanya kazi katika Bahari Kuu kama vile walivyosema kwamba meli ziwe zina ukubwa wa mita 34.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Serikali inunue meli kwa wingi na vijana wetu tuwahamasisha. Kwasababu vijana wamehamasika kufanya kazi kwenye boda boda tu, kila siku tunawaona wanavunjika miguu, wengine wanakufa. Lakini kama tutawahamasisha kikweli vijana wetu wana uwezo wa kusoma na wakapata vyeti vizuri na wakaweza kuajiriwa katika meli hizi ambazo zinavua katika bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pindi tukiridhia Azimio hili mi naona kwamba Azimio hili ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Vijana wetu watakapopata ajira watapungukiwa na umaskini na wataweza kupata ajira na kujiendeleza. Lakini na pia vijana watakapokuwa katika zile meli za nje wataweza pia kuwa ni walinzi wa mali zetu nan chi yetu pia kwa jumla. Kwasababu kule kutakuwa na mali zetu wanazona na wanajua kipi ambacho kinavuliwa na kuna mambo mengine ambayo sisi huku tutakuwa hatuyajuia lakini watakuwa kama ni walinzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kuridhia kwa asilimia 100 na nawaomba Wabunge wote waridhie Azimio hili kwa maendeleo ya nchi yetu na maendeleo ya vijana wetu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Kitwanga na Mheshimiwa Ruhaga Joelson Mpina ajiandae.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kabisa Azimio hili. Ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu tumelichakata sana jambo hili, tukishirikiana na Wataalamu wa Sekta ya Uvuvi na Wataalam wa Uchukuzi. Na kabla sijaendelea naomba nikupongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Kalemani naona wewe ni *shokup* na unafiti kote kote, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu, mimi yangu ni mawili tu. Naomba kwa namna ya pekee niwapongeze sana Wakuu wa Mikoa ya Tanga na

Mkoa wa Mara ambao walikasirika baada ya kuona nchi yetu inanyanyaswa, nami mwenyewe huwa napenda kuona watu wanakasirika nchi yetu inapokuwa inanyanyasika bila sababu za msingi, ambayo hatimaye imepelekea Marais wetu hawa wawili kuzungumza na hatimaye wakaweka mambo sawa. Vijana wale wamenikuna sana, hongera zao nyingi sana. Jamani walikuwa wanatetea watu wetu waliokuwa wanaonewa kwenye mipaka yetu kwenda nchi jirani, ndio ninachotaka kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme mambo mawili tu hili. Kwanza ni Azimio, kama tulivyoona faida zake ni nyingi sana kupitia maelezo, lakini kubwa kuliko ni jinsi ambavyo linakuja kuongeza nguvu kwenye sheria tuliyoitunga, Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Huko nyuma nikiwa katika Kamati hii ya Kilimo na Uvuvi tulipata semina muhimu sana na mtaalam mmoja kutoka Zanzibar, yule bwana mpaka leo namkumbuka; alitueleza namna ambavyo sisi ni *members* wa *MO* lakini bado hatujaridhia Mkataba huu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtalamu huyo alitueleza manufaa yake na kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wote tuliona manufaa yake ni mengi sana. Pia alitueleza jinsi ambavyo biashara ya tasnia hii ya uvuvi ilivyokuwa inasuasua Katika Bahari Kuu, jinsi tulivyokuwa tunaibiwa kwenye Bahari Kuu na jinsi ambavyo tulikuwa na vijana ambao hawana maarifa ya kutosha kwenye Bahari Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mkataba huu sambamba na sheria ambayo tumeipitisha, vinakwenda kujenga nguzo muhimu sana katika tasnia hii ya uvuvi na tafsiri yake pana ni kwamba tumewahi kusema kwenye Bunge hili kwamba kuna eneo lenye mapato mengi, lenye fedha nyingi ambazo ilikuwa hatujaliangalia, ilikuwa ni tasnia ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sheria hii na kuridhia Mkataba huu, tafsiri yake pana ni kwamba sasa tunakwenda kujielekeza kwenye chanzo kingine muhimu sana ambacho tulikuwa hatukitazami kama ni sehemu kubwa na muhimu sana ya mapato katika tasnia ya uvuvi.

Ziko nchi nyingi sana ambazo zimenufaika sana na tasnia ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo ningependa niliseme ni kuhusu madhara makubwa ambayo tungepata sisi ambayo ni kutoonekana kwamba bahari yetu siyo salama. Hilo lilikuwa ni jambo kubwa sana na hata huko nyuma nadhani hata Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi atakubaliana name. Ilikuwa vyombo vya nje vya Hong Kong, Thailand na kadhalika, vikija kuvua kwenye maji yetu tupolikuwa bado tunaonekana watu wetu hawana maarifa ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuridhia Mkataba huu, tafsiri yake ni kwamba ule mnyororo wa maarifa sasa katika tasnia ya uvuvi unakuwa umeboreshwa. Labda tu kwa Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi, hivi vyuo tunavifahamu, ni pamoja na Mbegani na Chuo kingine kipo Kigoma kule Kibirizi, amelisema vizuri sana huyu Mheshimiwa Dau kwamba lazima vyuo hivi tuviongezee nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo hivi vipo, vina wataalam wazuri, lakini lazima vyuo hivi tuviongezee nguvu. Lazima vyuo hivi tuviongezee vitendea haki na dunia ilikofika sasa hivi hata kama maana yake ni kupata maarifa kutoka nje kwa marafiki zetu ambao wanaweza kuja kutusaidia, kwa mfano, wakati wa semina ile Mheshimiwa Waziri utakumbuka yule mtaalam wa Zanzibar alitueleza kwamba wenzetu wa Serikali ya Norway ambao ni marafiki zetu wa kitamaduni (*traditional of rents*) walikuwa wameahidi kabisa kuendelea kutusaidia katika tasnia hii ya maarifa katika eneo hilo la uvuvi. Naomba vyuo vile viongezewe nguvu, viongezewe fedha, viongezewe vitendea kazi na wataalam wa kutosha ili vyuo hivi viweze kuwa na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Kibirizi ambacho ni chuo muhimu sana kinatazama hasa uvuvi katika Ziwa Tanganyika ni kweli bado kuna tatizo la vitendea kazi katika chuo kile. Itakuwa ni jambo jema sana tukijielekeza huko na Mheshimiwa Waziri tumepitisha Bajeti yako, tumeona fedha kwenye eneo hili la uvuvi ni za kutosha, basi zielekezwe huko

ili tasnia hii sasa iweze kujipambanua na ituongezee pato la Taifa katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni ulinzi na usalama wa watu wetu. Takwimu zinaonyesha kwamba takribani wavuvi zaidi ya 24,000 wanafariki kila mwaka katika maji yetu maeneo mbalimbali. Moja ya sababu ya vifo vyao ilikuwa ni udogo au uchache wa maarifa yao katika kuhimili vyombo vya baharini. Kwa kuridhia Mkataba huu, tafsiri yake pana ni kwamba tutakuwa na watu wenye maarifa zaidi, watafanya kazi kwenye meli hizi za kigeni na za kwetu wenyewe na wataweza kujiokoa zinapotokea shida katika maeneo haya ya bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, sisi Tanzania ni *member* wa *IMO*, tena ni *member* kweli kweli na yako mambo ambayo nina hakika sasa kupitia kuridhia Mkataba huu tutanufaika nayo kwa kiwango kikubwa sana..

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, nasema sisi kwenye Kamati tumepata semina, tumepitishwa na wataalam mbalimbali wa tasnia hii ya uvuvi, manufaa ni makubwa sana, tuwaombe Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kweli turidhie Mkataba huu ili tupige hatua kujiekeleza katika chanzo hiki kipya kabisa ambacho kitatungezea mapato katika nchi yetu. Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Ahsante sana na naridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Charles Kitwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Elias Kwandikwa, ajiandae.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amekuwa mlinzi na amenifikisha leo hii niweze

kuchangia azimio hili ambalo ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwa kusema kwamba kila mtu anayesimama, wengi wanasema tunazungumzia viwanda. Sasa mkataba huu ukiuangalia unazungumzia viwanda na meli ya uvuvi. Siyo meli ya kawaida tu, ndani yake kuna kiwanda, samaki wanapovuliwa wanaingia mle ndani wanafanyiwa machakato kukaa na ndani yake kuna mashine ambazo ni *very sophisticated* ambazo zinasaidia sasa kumweka huyo samaki katika hali ambayo mlaji wa mwisho anaifikia. Kwa hiyo, tunazungumzia mafunzo ya watu ambao wanapashwa wawe na uelewa wa hali ya juu, maana wako ndani ya meli ambayo ni ya kiwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania GDP yake kwa takwimu za mwaka 2019 ni *51billion* na ni ya 10 kwa Afrika ikiongozwa na Nigeria yenye GDP ya dola bilioni 376. Mkataba huu utatutoa hapo. *Opportunity* tulizonazo Watanzania ni kubwa mno kwenye eneo hili. Ikumbukwe kwamba ukichukua Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria, Tanzania inakuwa ndiyo ina maji baridi mengi kuliko nchi yoyote duniani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoa lile Ziwa lililoko Marekani, linalofuatia na lenyewe liko Tanzania. Kwa hiyo, hatuangalii tu uvuvi wa bahari, tunaangalia hizi meli za uvuvi katika nchi yake kwa ujumla, tukisharidhia sasa hili la Kimataifa sasa, twende chini tuangalie sheria zetu, Kanuni zetu na sera zetu ndani ya nchi ziende katika *standard* zile za Kimataifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa muda wa wiki kama mbili tumeona ndege ya *RwandAir* ikiruka kutoka Mwanza ikibena minofu ya samaki moja kwa moja. Sasa nijipendeleo na mimi; mtambue kwamba Wilaya au Jimbo linalopakana na Ziwa Victoria kwa urefu mkubwa zaidi ni Jimbo la Misungwi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri jirani yangu Jimbo la Nyamagana wana chuo cha kufundisha wavuvi. Sasa mafunzo yatakayokuwa yanatolewa hapo yaweze ku-*trickle down* yawezeshe hawa wavuvi wanaovua katika Ziwa Victoria wavue kisasa zaidi na bahati nzuri moja ya eneo lililopo jema sana katika Wilaya ya Misungwi au Jimbo la Misungwi ni eneo la Nyahiti ambalo ni mazalio ya samaki. Hawa wavuvi wakishapewa elimu nzuri, sina uhakika kama watakwenda kuharibu tena yale mazalia ya samaki ili wale samaki wanaovuliwa kutoka Ziwa Victoria waendeleo kuwepo na zile ndege ambazo zinakuja kuchukua minofu ya samaki pale uwanja wa Kimataifa wa Mwanza ziendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna mambo sana ambayo yamezungumzwa huku na ni-*declare* tu kwamba nami ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na niseme tu kwamba rafiki zangu wa uvuvi ni watu wenye elimu sana na watu wanaojua sana. Kwa sababu kuna mmoja alikuwa anataja hata idadi ya samaki na mayai ya samaki huko maziwani na huko sasa nikawa nashindwa kuelewa wenzetu wametuzidi kidogo na teknolojia ya kuhesabu mpaka samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ni jambo ambalo linafurahisha kwa sababu kama wajua hivyo ina maana *they are very considerate* kwenye *economy* ya nchi yetu na ndiyo sababu tumeungana nao na tumeshirikiana nao vizuri sana katika kuhakikisha kwamba sote tunakuja hapa kulitetea azimio hili ili lipite na uchumi wetu uzidi kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu nitoe ushauri kidogo. Kwanza pamoja na azimio hili kuja wakati ambao linahitajika, kwa sababu sasa tunaona uchumi wetu unaweza ukaongezeka zaidi ukatoka hiyo shilingi bilioni 51 kwenda zaidi kutokana na eneo hili. Waangalie mikataba mingine, maana wadau tuliowasiliza walizungumzia vilevile baadhi ya mikataba ambayo tunayo, lakini hatujairidhia na inaweza kuwa ni ya manufaa zaidi katika nchi yetu hasa katika eneo hili la uvuvi; siyo kwenye mafunzo tu, pia kwenye maeneo

mbalimbali. Basi naomba Serikali yetu ambayo kwanza ni sikivu na ambayo nina uhakika watatusikia... *(Kicheko)*

(Hapa simu iliita)

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Eeh, ajali kazini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa nasisitiza sana watu wasifanye hivyo, lakini leo bahati mbaya na mimi imenitokea. Kwa hiyo, nisamahe tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana basi, kama kuna mikataba mingine iletwe tuweze kuridhia na tuweze kuendana.

Sasa *this time* tuisubiri mahitaji yafike, bali tuwe *proactive*. Tuwe tumeridhia kwa sababu tumeshaangalia na kuona kwamba tuta-*benefit* na hiyo mikataba.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naona kengele ya kwanza imepigwa. Nimalizie tu kwa kukushukuru sana na niwashukuru sana wapiga kura toka Jimbo la Misungwi kwa *message* nyingi; nimepata zaidi ya *message* 2,800 za kuni-*encourage* niendeleo kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawataarifu wale ndugu zangu walioko mkono wa kulia, kule kuna mawe matatu. Ukija, yatakudondokea, msije; mkae huko huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kuniwezesha kutoa mchango wangu kwa njia hii ya maandishi.

Pili, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna anavyotuongoza hasa kwenye mapambano haya ya janga hili la Corona. Hakika miongozo yake ndio imetufikisha hapa, leo tunapoelekea kufungua shule zetu za *high level* na vyuo vyetu. Huu ni ushindi mwingine kwa nchi yetu hakika Mungu wetu anatupigania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Bunge lako litaridhia azimio hili itakuwa ni jambo jema sana kwani sasa ni muda muafaka wa kuridhia azimio hili, ukizingatia ni jana tu Bunge lako limetunga Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Hivyo utaona kuridhiwa kwa azimio hili kunakwenda sambamba na sheria hiyo. Kwa msingi huo naipongeza sana Serikali kwa kuleta azimio hili leo kwani sasa taasisi zetu zitafanya kazi huku zikitambuliwa hata na taasisi za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwenye maudhui ya azimio lenyewe linakwenda kupanua wigo kwenye ufanisi wa vyombo vyetu mbalimbali vya baharini ikiwa ni pamoja na kupandisha viwango vya wafanyakazi wa sekta hii kama vile mabaharia na makepteni wetu. Pia katika hili naomba sana kwenye utekelezaji wa azimio hili suala la lugha ya kiswahili ni bora sana ikajumuishwa kwenye azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuridhiwa kwa azimio hili suala la kuimarisha vyuo vyetu vya uvuvi ni muhimu sana ili kwenda sambamba na azimio lenyewe. Kwa kuwa sasa tunaingia kwenye viwango vya kimataifa, ni lazima vyuo vyetu viwe na mitaala ya kimataifa ili kukidhi matakwa ya azimio hili. Ili Taifa letu lisiwe wasindikizaji katika itifaki hii ni lazima kuwe na maandalizi makubwa ya kisasa ikiwemo na ile ya ujenzi wa bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli za uvuvi

wa bahari kuu ili kuendana na itifaki hii. Kuwa na vifaa vya kisasa ni muhimu sana ili tusipitwe na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo sasa naomba kuunga mkono hoja 100%.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wote wa Taifa letu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuijalia nchi yetu mafanikio ya ustawi wa kijamii, kisiasa, kiuchumi, kidiplomasia na huduma bora kwa wananchi. Nikianza kwa Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa pamoja tunasema ahsante sana Mwenyezi Mungu sisi sote tu waja wako, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaasa Watanzania wote kuungana katika kuliombea Taifa letu kwa Mwenyezi Mungu kuhusu janga hili la Corona linalohatarisha ustawi wa jamii kwa Taifa na dunia nzima hakika ugonjwa huu ni hatari sana. Hivyo basi sote tuungane kwa kupambana na ugonjwa huu kwa kuzingatia maelekezo, kanuni ya Wizara ya Afya nyakati zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa jinsi ilivyotekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2015 - 2020. Hakika tuko kidedea kuelekea uchaguzi Oktoba, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe mchango wangu wa kuishauri Serikali kupitia kwanza binafsi nasema Watanzania tuendeleo kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuijalia nchi yetu urithi wa ukanda mkubwa wa bahari kuu. Aidha, naipongeza sana Serikali yetu kwa kuandaa mkataba huu ambao ni muhimu sana kwa Taifa letu na ustawi katika tasnia ya uvuvi wa mazao ya bahari kuu. Hivyo basi Serikali yetu iweke mkakati wa kuandaa wataalamu wabobezi kwa ajili ya kusimamia shughuli za bahari kuu.

Pili, Serikali itazame kwa upana mazingira ya uvuvi shindanishi katika viwango vya kimataifa pamoja na kwamba huu ni mkataba tunaouridhia kama nchi mbele ya mataifa ni muhimu kwa maslahi mapana kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwa kuwa mkataba huu ni azimio lenye lengo la maridhiano ya kuweka mazingira ya kulinda, kuhifadhi, kutunza ustawi wa rasilimali yenye kunufaisha pande zote hivyo basi Serikali iweze kuelimisha wadau mbalimbali na kukuza taaluma mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa 100% na naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Luhaga Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa na Mheshimiwa Medadi Kalemani, ajiandae.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri aliyewasilisha Mkataba huu pamoja na Kamati iliyohusika na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Mawasiliano kwa ujumla wake kwa jinsi ambavyo wameandaa vizuri sana Muswada huu na kuwasilisha leo kwenye Bunge lako. Nikiri kwamba Wizara yangu imehusishwa katika hatua zote za ukamilishaji wa maandalizi ya Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia katika Muswada huu ambao wameeleza mambo mengi, lakini kilichotufurahisha kikubwa kabisa ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wanaunga mkono Mkataba huu kwa nguvu zote na kutuambia kwamba tulichelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuliambia Bunge lako kwamba limeingia kwenye *record*. Kwa kweli miaka mingi watu wamezungumza kuhusu Uvuvi wa Bahari Kuu, lakini Bunge hili Waheshimiwa Wabunge mmeingia kwenye *record*

kwa utashi wa dhati kabisa wa kuhakikisha kwamba mambo sasa, rasilimali zetu zilizopo katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, sasa Taifa letu litanufaika nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmethibitisha hili; moja, kwa jana kwa kukubali kutunga Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, 2020 ambao jana mmeipitisha kwa kishindo na vile vile mmeipitisha Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari ambalo na lenyewe ni Bunge hili liliupitisha Mkataba huo; na leo mnaenda kupitisha Mkataba wa Kimataifa wa viwango vya mafunzo na utoaji wa vyeti vya wafanyakazi na vyombo vya uvuvi ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo matatu yote ambayo mmeyafanya sasa yataliwezesha Taifa kunufaika na rasilimali zake za uvuvi wa Bahari Kuu. Sasa kuna vitu vingine ambavyo ni viporo vimebaki vya kumalizia hapa ambavyo ni Sera ya Uvuvi. Waheshimiwa Wabunge hapa wameuliza kuhusu Sera ya Uvuvi kwamba iko wapi? Sera ya Uvuvi wa Bahari Kuu iko wapi au Sera ya Uvuvi wa Bahari iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachoweza kusema hapa ni kwamba tunafanya maandalizi, hatukuwa na Sera ya Uvuvi wa Bahari Kuu na sasa Serikali iko kwenye maandalizi ya kuandaa hii Sera ya Uvuvi wa Bahari Kuu na kuanza kutumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni eneo hili linaloenda sambamba. Mikataba hii na sheria hizi tulizoziunda zitagusa hata kuanzishwa kwa sheria au kufanya marekebisho ya baadhi ya sheria nyingine. Hata huu Mkataba mnaoupitisha unaweza ukagusa baadhi ya sharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, kwa sheria tuliyoipitisha jana, eneo kubwa litakaloguswa na kuanzishwa kwa Mkataba huu litakuwa ni eneo la Kanuni ambalo nalo tutalisuka kwa utaratibu ambao utawezesha kutekelezwa kwa Mkataba huu kikamilifu. Katika kufanya hivyo tutahakikisha wenzetu wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

tunawashirikisha kikamilifu ili tuweze kutoka na Kanuni ambazo zinaweza kulisaidia Taifa letu kupiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuboresha Vyuo vyetu imezungumza hapa, lakini ikazungumzwa na jinsi vijana wetu, siyo kwamba walishindwa kabisa kufanya ila walikuwa wanachoka kwa yale mawimbi. Hilo nakubali kwa sababu kama ambavyo mafunzo tunayatoa ni kwamba ilikuwa yalikuwa yanaishia utoaji wa meli zenye urefu wa mita 23. Kwa hiyo, katika mawimbi marefu vijana wetu bado hawajawa na mazoezi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia Mkataba huu, mimi kwa dhamana ya Wizara yetu na kwa dhamana ya Serikali na kwa kushirikiana tutahakikisha kwamba vyuo vyetu tunaviboresha ili tuweze kutoa wataalam wenye weledi ambao wataweza kusimamia katika maeneo yote ya maji ya kawaida lakini na eneo la Bahari Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamelizungumza suala hili nasi tunasema kabisa kwamba tunalichukua kuhakikisha kwamba zana zile zinazotumika kufundishia zitapelekea vijana wetu kupata mafunzo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vyetu hivi vinaheshimika kwa kweli na hata kwa majirani zetu. Kila mwaka wanakuja vijana wa kutoka nchi mbalimbali zaidi ya 25 kuja kujifunza, kuja kuchukua *course* mbalimbali hapa nchini kwetu. Kwa hiyo, kwa marekebisho haya tutahakikisha sasa wataendelea kuja wengi zaidi hapa nchini kuchukua mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, sasa hivi tunatoa wanafunzi kila mwaka kama 1,000 tu. Tunaenda sasa kuwa na uwezo wa kutoa wanafunzi wengi zaidi kwa mwaka kutokana na maboresho ambayo tutayafanya katika hivi vyuo vyetu ambavyo vitawezesha kwa kweli kupiga hatua kubwa sana katika eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni nini maandalizi yetu katika mkataba huu baada ya kuidhinishwa leo na Bunge kubariki kuidhinishwa kwake. Cha kwanza kabisa kama tulivyosema tutahuisha baadhi ya sheria ambazo zitaguswa; Tutapitia mitaala ya *FETA* upya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba yale yaliyoko kwenye mkataba yote yamezingatiwa; Kuandaa wataalam, kwasababu tutapanua sana uandaaji wa wataalam katika haya maeneo; na Kuandaa vifaa vya kufundishia kama nilivyosema. Hayo yote tutazingatia katika utaratibu wa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge kwamba Vyuvo vyetu hivi ni kweli kwamba vilikuwa vinashindwa kutoa wataalam na vyeti vyake vilivyokuwa vinatolewa kwasababu hatukuwa na ithibati ya *IMO* vilikuwa haviwezi kutambulika Kimataifa. Sasa leovyeti vyetu vinakwenda kutambulika Kimataifa duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza uvuvi wa Bahari Kuu wakati tulikuwa na uwezo wa kufundisha vijana kuishia mita 23 na Bahari Kuu kwa kweli ni kuanzia mita 24 na kuendelea. Tutaweza kuingia huko kwenye uvuvi wa Bahari Kuu bila tatizo lolote na nyongeza ya hapo ni kwamba *DSFA* walikuwa wanakosa vijana kwa ajili ya kusimamia shughuli za uangalizi wa meli zinavyokuja kama Wabunge walivyozungumza, sasa tunakwenda kulisimamia lile eneo kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kama utaniruhusu, ni hili ambalo limezungumza juu ya ukamataji wa kiholela. Tumeuleta huu mkataba kuridhiwa tukiamini kwamba sisi hakuna mahali au siku moja tuliyoweza kumkamata mtu yoyote au meli yoyote kiholela. Meli zote tunazikamata kwa mujibu wa sheria na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge mtaungana nami kwamba, toka tumeanzisha haya mapambano ya uvuvi haramu, tumekamata wavuvi haramu zaidi ya 4,000 na katika hao 4,000, zaidi ya 150 tuliwapeleka Mahakamani. Katika zile kesi 150 tulizopeleka Mahakamani hatujawahi kushindwa kesi

hata moja. Hiyo yote ni uthibitisho kwamba hatufanyi mambo haya kwa kukurupuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, vijana hao watiwe moyo wanapozifanya hizi kazi na sehemu ya kutiwa moyo ni hapa kwenye Bunge, kwasababu kama wanafanya kwa nia njema basi nia njema ibaki hiyo hiyo. Jana nilieleza kuhusu hii Meli ya Magufuli, manufaa tuliyoyapata baada ya kuikamata hiyo meli ni makubwa mbona hayapongezwi? Mbona kila siku ni Meli ya Magufuli, Meli ya Magufuli kwanini zile faida za Kitaifa hazipongezwi? Hapo ndiyo ulikuwa mwanzo wa Taifa hili kwenda kunufaika na mazao ya uvuvi na rasilimali za uvuvi hapa nchini, sasa tutende haki, tuwatendee haki hawa vijana, tuwape moyo, lakini kuwa-*crush* tu kwamba wanakamata kiholela, wanakamata kiholela, sasa mwisho wa siku utamtuma nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, waende wakafanye hizo kazi, mtu akivunja sheria kwenye nchi hii atakamatwa. Suala la Mahakamani imekuaje, hilo lingine lakini mtu yoyote atakayevunja sheria za nchi yetu atakamatwa na vijana hawa wapewe uwezo na watiwe nguvu ya kuendelea kuwakamata wahalifu wote ili rasilimali zetu hizi za uvuvi ziendeleo kuwanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Elias Kwandikwa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Merdad Kalemami

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mungu kwa kutupa afya njema sote na ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako ili nipate nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii muhimu. Naunga mkono asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia niwashukuru Kamati tulifanyakazi vizuri kwenye Kamati na

nimshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kakoso na Makamu wake, Mheshimiwa Hawa, kwasababu tulivyokutana kwenye Kamati na hata tulipokuwa na wadau ambao tulikuwa na *TASAC*, tulikuwa na *FETA*, tulikuwa na *DMI*, tulikuwa na wataalam wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, lakini pia tulikuwa na Chama cha Wafanyakazi wa shughuli hizi za uvuvi, tulikuwa na mijadala mizuri sana, Wajumbe wa Kamati watakuballiana nami. Kwahiyo, niwapongeze na kuwashukuru sana kwa ushirikiano ambao walitupa kwenye kujadili juu ya azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa namna ulivyoongoza mjadala huu na tumeshuhudia hapa Wabunge karibu wote wamepongeza kwa hatua hii, kwaiyo nakushukuru sana. Pia nimshukuru Mheshimiwa Spika na viongozi wa Bunge kwa ujumla kwasababu tunaona chimbuko la azimio hili ni pamoja na ile Tume ya Mheshimiwa Spika aliyoiunda na hatimaye jana tumepata sheria nzuri kabisa ambayo itakwenda kusimamia uvuvi wa bahari kuu na naamini azimio hili pia litakwenda kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa sheria hii ambayo jana tumeipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu machache ambayo wachangiaji waliyazungumza hapa na nianze kwanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Luhaga Mpina kwa kutoa ufafanuzi wa mambo kadhaa yaliyozungumzwa hapa. Mheshimiwa Mpina namshukuru sana na inaonyesha namna ambavyo Wizara yetu pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunavyoshirikiana kwenye hatua zote na naamini kabisa tutaendelea kushirikiana kwasababu ametaja juu ya Sera ya Bahari. Nafahamu kwamba katika uundaji wa Sera hii ya Bahari tunashirikiana kuhakikisha kwamba tunakuja kuwa na Sera mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu hapa limezungumzwa suala la matumizi ya Kiswahili na najua hata kwenye Kamati tulizungumza, sisi tumelichukua kwa kulifanyiakazi kwasababu tunaona uko umuhimu wa kuona tunalisukuma suala hili ili liveze kuwa sehemu inayostahili. Kwahiyo suala la matumizi ya Kiswahili tunakubaliana na

Kamati, tunaendelea kulifanyiakazi tuone kwamba tunafanya namna nzuri ya kuona Kiswahili chetu kinatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na ushauri hapa wa kununua vifaa. Nikiri tu kwamba siyo muda mrefu sana tumekuja na Sheria ya *TASAC* lakini kwa lengo hilo hilo la kuona kwamba tunakwenda kuboresha ule udhibiti wa shughuli za majini. Kwahiyo, pamoja na mambo mengine unaona kabisa tumejipanga kuja na meli ya uvuvi, lakini pia kuhusu vifaa tutakuja pia na meli ambayo itaweza kubeba wataalam kwa haraka kwasababu mtaona kwenye azimio hili tunakuja na wataalam ambao kwa ajili ya udhibiti ili kuona ule usalama, kukagua vifaa na kadhalika. Kwahiyo lazima hawa wataalam wawe na chombo cha kuwawezesha kwenda kufanya shughuli zao ili iweze kuleta mantiki. Kwahiyo, hili nalo tunakwenda nalo ili kuhakikisha kwamba wakati tunaboresha taasisi yetu ya udhibiti lakini pia tunawawezesha kuwa na vifaa ili waweze kupata vyombo vya kuwapeleka kufanyakazi huko ndani ya Bahari lakini pia kuwepo na vifaa vya ufundi kama tulivyozungumza *technical equipments*, lakini pia naasuala yale ya usalama. Kwahiyo, yote haya tumeona kwamba nilazima tuyasukume kwa haraka ili wakati tunatekeleza Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu lakini lazima tuone ule udhibiti unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Luhaga Mpina pia alijaribu ku-*respond* kwenye hoja ya Ndugu yangu Kiwanga hapa. Nimtoe wasiwasi kuwa sheria hizi zipo nyingi, kikubwa sana ni kusimamia sheria na sisi kama Serikali tunajipanga kuona kwamba tunazisimamia vizuri sheria ili kutokuacha huuupungufu ambao unaweza ukajitokeza kuona kwamba azimio kwa mashaka aliyokuwa nayo kwamba labda linaweza kwenda kuwa *idle*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, azimio hili limekuja kwa wakati muafaka, ndiyo maana hata wachangiaji walivyoanza, Mheshimiwa Ramo Makani alizungumza hapa kwamba je, tumechelewa? Ni maswali ambayo hata kwenye Kamati tulikuwa tunajuliza, lakini sisi tunaona kwamba limekuja wakati muafaka kwasababu

wakati huu tunakwenda kwenye uchumi wa kati tunazungumza juu ya kuwa na meli kubwa za uvuvi hii ambazo kimsingi ni kiwanda cha samaki. Kwahiyo, unaona sasa tunahitaji kufanya udhibiti kwa sasa mahitaji hayo huu ndiyo muda wenyewe. Kwahiyo mahitaji yetu ni kwenda kuona kwamba sasa tunavutia kuwa na meli za kigeni ambazo pia tutadhibiti ili kuweza kupata manufaa makubwa bila kupoteza hata mapato ya Serikali, kwahiyo, tumejipanga hivyo. Kwa hiyo, azimio limekuja wakati mzuri ambao sasa tunakwenda kusukuma kuona kwamba maendeleo yanakwenda kutuletea mazao makubwa kule baharini na tuweze kufanya vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie, nasikia kengele ya kwanza; niseme kwamba, iko mifano ambayo tunaishuhudia kwa wale ambao tayari wamesharidhia mkataba huu. Nataka nitolee mfano tu Afrika ya Kusini ambao tayari wamejiunga, ziko faida zake ambazo wamezipata ikiwani pamoja na kuona kwamba wale wafanyakazi tunalenga kuwapa mafunzo na kupata vyeti wanaweza sasa kwenda kufanya vizuri. Mheshimiwa Dau hapa alitolea mfano kwamba wale ndugu zetu walikuwana mafunzo, labda hawakufanya mazoezi ya kukaa kwenye Bahari Kuu wakaingia baharini wakaishia kutapika na kulala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Dau kwamba, azimio hili litakapokuwa limepitishwa na mafunzo kwenda kulekelezwa tutafanikiwa pia ili kuona kwamba wale watu wetu tunaowafundisha wanapata mazoezi ya kutosha, wanapata uzoefu, lakini meli za kigeni tutaweza kuzitumia kufanyia mafunzo ili hawa wakipata vyeti tayari wawe pia na uzoefu wa kwenye mafunzo wa kuweza kukaa baharini na watakapokuwa wamerudi watafanyakazi bila kuwa na mashaka. Kwahiyo, nilitaka nimtolee ule mfano wa Afrika Kusini kwamba vyo vyake vya uvuvi vilivutia wanafunzi wengi wa kigeni kupata fursa ya mafunzo kwa vitendo katika vyombo hivyo vya uvuvi vya kigeni. Kwa maana hiyo sasatatizo kama hilo walilopata wenzetu lililotolewa mfano halitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hiyo ya Afrika Kusini imepata mafunzo, fedha, wataalam na utalam kutoka nchi za kigeni. Kwa maana hiyo, yapo manufaa yatakatotokana na kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa nafasi hii. Nimalizie kwa kumpongeza sana mtoa hoja kwa kutoa na kuwasilisha hoja vizuri sana. Kwa kweli sina cha kusema Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwaasilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nimkaribishe sasa Dkt.Merdad Kalemani, Waziri wa Nishati kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, mtoa hoja ahitimishe hoja yake.

WAZIRI WA NISHATI -K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja yangu. Kabla sijahitimisha napenda niwashukuru sana wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika kwa michango na miongozo mizuri katika mjadala huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge waliochangia nitakribani 12 waliochangia kwa hoja ya kuzungumza na baadhi wamelata michango yao kwa maandishi. Kwahiyo hoja hii imejadiliwa na kuungwa mkono kwa asilimia mia moja na wote wamechangia kwa kukubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba nitoe shukurani kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Kamwelwe aliyepata udhuru; Waheshimiwa Manaibu Waziri wote wawili, wamefanyakazi vizuri sana, wamenipa ushirikiano; Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii na hata mimi mwenyewe nimefanyakazi vizuri ndani ya dakika chache zilizopita kwa kushirikiana na wengine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mpina kwa ufafanuzi wa kina alioutoa hivi karibuni kuhusiana na masuala ya kisera na usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo saba ya ujumla yaliyozungumzwa. Kabla ya hoja hizo saba nitangulie kusema, kwanza mkataba huu wa Bahari Kuu Duniani ulianzishwa Mwaka 1948, tangu sisi tukiwa chini ya usimamizi wa Mkoloni na mwaka 1974 Serikali yetu ikajiunga, lakini hatukuweza kufanya mambo ya mafunzo na utoaji wa vyeti kwa wavuvi. Leo ni takribani miaka 47. Tunaipongeza sana Serikali hii kwa kupitisha azimio hili na kulileta Bungeni ili liweze kuridhiwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nitangulie pia kusema hadi sasa, kati ya nchi 174 duniani, nchi 32 zimeshajiunga kufikia tarehe 15 mwezi huu na Tanzania kwa heshima ya Bunge lako Tukufu dna sisi tunakwenda kutekeleza maazimio haya ya mafunzo na utoaji vyeti. Ni hatua kubwa sana ambayo tutaifikia kama Bunge lako likiridhia.

Kwa hiyo, nasi tuko katika hatua nzuri hatujachelewa. Nchi za Afrika ambazo zimeshajiunga ni pamoja na Uganda, Siera Leone, Congo, Gambia, Tunisia pamoja na Afrika Kusini, kwahiyo sisi kujunga ni hatua kubwa sana ya kupongeza. Tuipongeze sana Serikali yetu kwa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa suala la lugha ya Kiswahili; nipende kusema na kuishukuru Serikali yetu, kwanza kimsingi Serikali yetu ilishaanza kuchukua hatua kabisa kubwa za kuhakikisha lugha ya Kiswahili inaingia katika lugha za Kimataifa ili iweze kutumika. Bahati nzuri katika mkataba huu mkisoma Waheshimiwa Wabunge, aya ya 10 ya mkataba huu inaruhusu kufanya maboresho yaliyomo kuingiza chochote mnachotaka ilimradi muwasilishe taarifa kwa wakati huu mkiwa/MO. Sisi tutatumia nafasi hii ya mkataba huu ili Kiswahili nacho sasa kiweze kuingia katika mikataba hii ya Kimataifa ya Bahari Kuu, ikimpendeza Mungu.

Kwahiyo, tutatumia nafasi hii, kifungu hiki ili kuweza kuingiza lugha ya Kiswahili na wenzetu wakiridhia *Insha Allah* itaweza kutumika mbele ya safari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la kuongeza ujuzi na ubora; ndiyo maana tumeingia katika itifaki hii. Tunavyo vyuo vitano kama ambavyo mmeona vya Bagamoyo, Kibirizi kule Kigoma, tunacho cha Nyegezi, Mwanza; tunacho cha Rorya; na tunacho cha Mtwara-Mikindani. Hata hivyo, vyuo hivi kimsingi vinatoa *certificate* (vyeti), sasa tukiingia katika mkataba huu tutaingia katika muskabali wa kuweza kuwa na viwango vya juu vya wataalam wetu ili nao waweze kubobea katika usimamizi wa masuala haya. Kwahiyo, Waheshimiwa Wabunge wakipitisha sisi ni matumaini yetu tunakwenda kuongeza uwezo wa wataalam wetu lakini pia kujenga uwezo wa vyuo tulivyonavyo napengine kufanya upanuzi zaisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameeleza Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi hapa, hivi leo tunatoa wanafunzi takribani 1,000 kwa mwaka. Mpango wetu ni kuongeza mara mbili ya wanafunzi wanaohitimu kwa sasa na kwa viwango vya juu na vya Kimataifa, itifaki hii ikishapita. Kwahiyo, nalishukuru Bunge kwa kujadili hoja hii na *Insha Allah* itapitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusiana na Sheria na Kanuni; nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri Mpina jana tulipitisha sheria hii, lakini pia ni matumaini yetu baada ya kuidhinishwa na kutumia utaratibu wa Kikatiba na mkataba huu, basi tutakwenda kuyatarisha kanuni ili kurahisisha utekelezaji wa mkataba huu kadri utakavyofika wakati wa utekelezaji. Bahati nzuri sana kuanza kutumika kwa mkataba huu ni miezi 12 baada ya kuridhiwa na Nchi Wanachama 15. Bahati nzuri nchi 32 zimesharidhia, kwahiyo wakiridhia Waheshimiwa Wabunge tunakwenda kutekeleza itifaki hii haraka iwezekanavyo kwa sababu akidi tayari imeshatimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni manufaa ya itifaki hii. Tumeona

inakwenda kuongeza ajirana kuongeza uwezo wa wataalam wetu. Vyuu tulivyonavyo kwa kiasi kikubwa vinafundisha lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Tunakwenda sasa kuwafundisha wataalam wetu lugha za Kifaransa, lugha yetu ya Kiswahili ndiyo itakuwa mhimili wenyewe na lugha nyingine za Kimataifa ili wasibabaike katika kusimamia masuala haya inapojitokeza mahitaji kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo manne yamezungumzwa kwenye suala la usimamizi; kabla ya itifaki hii kuna *ILO*, kuna *FAO* na Mashirika mengine duniani na yote kila moja lina mustakabali wake wa kuzungumia masuala haya. Waheshimiwa Wabunge, wataona bilashaka kwamba mwaka 1994, *IMO* inaonyesha kwamba kuna wavuvi zaidi ya 24,000 hupotezamaisha kwa kutozingatia taratibu. Hii ilikuwa ni kwasababu ya kutokuwa na *international standards*, lakini tukienda kukidhi jambo hili, masuala kama haya yatapungua sanana wataalam wetu watafanyakazi kwa ufanisi. *ILO* inaonesha kwamba watu wanafanyakazi bila kuzingatia taratibu za ajira hasa wavuvi katika Bahari Kuu, sasa kwa kupitisha itifaki hii inakwenda kuondoa tatizo hilo na kuleta manufaa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwasababu Wabunge wanahitaji tupitisha jambo hili kwa haraka na wengi wameonesha tumeshachelewa, nisingependa niwacheleweshe, naomba basi nitoe hoja ili Waheshimiwa Wabunge tuweze kupitisha jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995F Liliipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Naona kuna Wabunge wanamsisitiza Mheshimiwa Susan Kiwanga asimame. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge kwa kawaida na kwa mujibu wa Kanuni zetu nilitakiwa niwahoji, sasa kwa utaratibu tunaoutumia sasa wa kupiga kura, nilikuwa natazama kura hapa zimeshapigwa na Wabunge wengi kabisa wa kutosheleza na Wabunge wengi wameridhia mkataba huu upite. Kwahivyo, Waheshimiwa Wabunge Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995F (*International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995F*) limepitishwa rasmi na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa uratatibu wetu Bunge limemaliza sehemu yake ya kuridhia na sasa tunarudisha kazi kwa Serikali ikaendeleo na michakato yake kuangalia sheria ambazo itabidi zibadilishwe kwasababu ya Bunge kuridhia mkataba huu na pengine na kanuni mbalimbali ambazo zilikuwepo zikifanyakazi lazima mwangalie mkataba huu unasema nini na sisi kwasababu tumesharidhia muangalie hayo yote na naamini Bunge litakuwa tayari kupitisha sheria nyingine ama mabadiliko yoyote yatakayotakiwa ili kuhakikisha mkataba huu ambao kimsingi umeungwa mkono na Wabunge wote uweze kufanyakazi ile ambayo imekusudiwa.

Tunaipongeza Serikali kwa hatua hiyo, lakini pia nalishukuru Bunge hasa kupitia Kamati yetu ya Miundombinu kwa kazi nzuri sana waliyoifanya ya kupitia mkataba huu ambao umetupelekea kwenye Bunge kuazimia kuridhia mkataba huu, tunawashukuru sana. Vile vile Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kuchangia kwa maandishi na wengine wamechangia kwa kusimama hapa ndani, tunawashukuru sana. Naamini mawazo mengi mliyoyasema mengine kama siyo ya kuhusu mkataba basi yatawasaidia Serikali katika kuhakikisha mkataba huu unatekelezwa ipasavyo.

Baada ya kusema hivyo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 8.00 mchana.

*(Saa 10.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 22 Mei, 2020 Saa Nane Mchana)*